**Kikao cha Tisa – Tarehe 24 Februari, 2021**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, katika kikao cha Baraza cha tarehe 15 Februari, 2021 Mhe. Anna Athanas Paul aliuliza swali la nyongeza lililotokana na swali la msingi Nam. 8 na Mhe. Kaimu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais aliahidi kujibu swali hilo kwa maandishi.

Vile vile, katika Kikao cha Baraza cha tarehe 16 Februari, 2021 Mhe. Miraji Khamis Mussa aliuliza swali la nyongeza lililotokana na swali la msingi Nam. 86 na Mhe. Kaimu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais aliahidi kujibu swali hilo kwa maandishi.

Aidha, katika Kikao tarehe 12 Februari, 2021 Mhe. Nassor Salim Ali aliuliza swali la nyongeza lililotokana na swali la msingi Nam. 9 na Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji alihidi kujibu kwa maandishi.

Sasa nawaomba Mhe. Kaimu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji wasome majibu ya maswali ya nyongeza yaliyoulizwa na Wajumbe hao. Ahsanteni.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi (Kny. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais):** Mhe. Spika, naomba kukiri kwamba tarehe 15 Febuari, 2021, wakati nikijibu swali la msingi nam. 8 lililoulizwa na Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis kuhusu kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo wa Watu Wenye Mahitaji Maalum, kutokana na majibu yangu Mhe. Anna Attanas Paul aliuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Je, ni vikundi gani vilivyonufaika na mikopo inayotokana na mfuko wa Maendeleo kwa Watu Wenye Mahitaji Maalum.

b) Je, vikundi hivyo vipo sehemu gani.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha majibu kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, vikundi vilivyo nufaika na mikopo inayotokana na Mfuko wa Maendeleo kwa Watu Wenye Mahitaji Maalum ni vitatu (3). Vikundi hivyo vyote vipo Unguja, ambavyo ni:

1. Na Sisi Tuwe Mbele - Mpapa

2. Maftani na Maendeleo - Tunguu
3. Ushirika wa Walemavu - Fukuchani

Mhe. Spika, kwa upande wa Pemba vikundi viliwasilisha maombi, lakini vikundi hivyo kwa bahati mbaya havikukamilisha utaratibu na havikukidhi vigezo. Vikundi vyote hivyo vimeelekezwa kuchukua hatua ili kufikia vigezo vilivyowekwa navyo viweze kunufaika na mikopo hii.

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi au kuna majibu zaidi. Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kumradhi. Mhe. Kaimu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais anaendelea kidogo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi (Kny. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais):** Mhe. Spika, Tarehe 16 Febuari, 2021 wakati nikijibu swali la msingi nam. 86 lililoulizwa kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Fatma Ramadhani Mohamed Mhe. Miraji Khamis Mussa aliuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

a) Je, serikali kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ilibahatika kukusanya kiasi gani katika maeneo yaliyochimbwa mchanga Mkoa wa Kaskazini Unguja.

b) Je, serikali imechukua hatua gani kwa maeneo hayo yaliyochimbwa mchanga na tozo yake imeshachukuliwa katika kurejesha ardhi hiyo kimazingira.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu maswali hayo kama ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, Jumla ya maeneo matatu (3) yalichimbwa mchanga kwa mwaka 2019/2020 kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja. Maeneo hayo ni Pangatupu, Fujoni na Kidanzini.

b) Mhe. Spika, kwa shughuli hiyo ya kuchimbwa mchanga katika maeneo hayo, serikali ilikusanya jumla ya shilingi bilioni nne, milioni mia tatu thamanini na nne, laki sita na thalathini na tatu na mia nne (4,384,633,400/=) ikiwa ni mapato ya uchimbaji mchanga huo. Fedha zote hizo ziliingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, kikawaida kwa kila tani moja (1) ya mchanga inatozwa jumla ya 6,500/= ambazo zimegawanyika kwa mchanganuo ufuatao:

| Na. | Aina ya Mgao | Kiwango (TZS) |
|---|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Serikali ya Mitaa | 1,000/= |
| 2. | Ada ya Uchimbaji | 1,500/= |
| 3. | Ada ya Usafirishaji | 1,000/= |
| 4. | Ada ya urudishaji wa eneo | 1,500/= |
| 5. | Fidia | 1,000/= |
| 6. | Gharama za uendeshaji | 500/= |

| | | |
|---|---|---|
| | Jumla | 6,500/= |

Mhe. Spika, kwa mchanganuo huo, wastani wa asilimia wa 23 ya tozo la mchanga inatumika katika kurejeshea maeneo yaliyochimbwa. Hivyo, kwa mapato ya jumla ya shilingi 4,384,633,400/=, fedha za urejeshaji ni shilingi 1,008,465,682/= kwa maeneo yote matatu.

Mhe. Spika, hadi hivi sasa eneo moja tu la Kidanzini ndio lililoendelezwa kwa kupandwa miti. Serikali inaahidi kuyaendeleza maeneo yaliyobakia hatua kwa hatua kupitia Idara ya Nishati na Madini, Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka na pia kwa mashirikiano na Wizara ya Fedha na Mipango.

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

**Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante, Mhe. Spika, naomba kuwasilisha gharama za matengenezo ya MV Maendeleo iliopo Mombasa, ambazo gharama hizo zilitakiwa na Mhe. Nassor Salim Ali. Mhe. Spika, gharama za matengenezo za MV Maendeleo zimegawika katika sehemu tatu, nazo ni:

**1. Gharama za Matengenezo ya Umbile la Meli**

Kazi ya matengenezo ya umbile la meli inafanywa na Kampuni ya *African Marine* iliyoko Mombasa Kenya na gharama za matengenezo hayo ni Dola za Kimarekani Laki Tano Elfu Nne Mia Tano na Thamanini na Nne na Senti Thelathini na Tano (*USD* 504,584.35).

**2. Gharama ya Ununuzi na Ufungaji wa Mitambo**

Kazi ya ufungaji wa mitambo inafanywa na Kampuni ya *Kyros Engine Solution* ya nchini India kwa gharama ya Dola za Kimarekani Laki Mbili Hamsini na Tisa Elfu na Mia Tano (*USD* 259,500).

**3. Gharama za Vifaa vya Uokozi**

Kwa upande wa gharama za vifaa vya uokozi Shirika la Meli linahitaji Dola za Kimarekani Laki Mbili Sabini Elfu na Mia Nane (*USD* 270, 800) kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo.

Mhe. Spika, Jumla ya fedha zinazohitajika kukamilisha matengenezo ya MV Maendeleo ni Dola za Kimarekani Milioni Moja Thelathini na Tano Elfu Mia Moja Themanini na Nne na Senti Thalathini na Tano (*USD* 1,035,184.35). Ahsante, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**Mhe Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, naomba kuweka Hati Mezani kuhusu Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani yake. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:** Mhe. Spika, kwa heshima naomba kuweka Hati Mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia

Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani yake. Mhe. Spika, kwa heshima naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

## MASWALI NA MAJIBU

### Nam. 76

### Ujenzi wa Barabara ya Wawi Mabaoni Kupitia Skuli ya Dkt. Omar

**Mhe. Bakari Hamad Bakari** - Aliuliza:-

Barabara ya Wawi Mabaoni kupitia Skuli ya Dkt. Omar ni ya muda mrefu na ina historia kubwa sana katika nchi yetu. Barabara hii ni mbovu na inaleta usumbufu mkubwa sana kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuikarabati barabara ya Mabaoni angalau kwa kiwango cha kifusi.

(b) Je, serikali inachukua hatua gani katika kuondosha changamoto hii kwa barabara za ndani zilizopo katika jimbo la Wawi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la Mhe. Bakari Hamad Bakari swali lake Nam. 76 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, barabara ya Wawi Mabaoni tayari imeshafanyiwa upembuzi yakinifu na Michoro yake imeshaandaliwa. Ujenzi wa Barabara hiyo utafanyika pindi hali ya kifedha itakaporuhusu, kwani fedha zinazotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za ndani ni kidogo kulinganisha na mahitaji yaliyopo.

Mhe. Spika, serikali kwa sasa inaendelea na hatua ya kuzifanyia utambuzi barabara zote za ndani katika Jimbo la Wawi na Majimbo mengine ya Unguja na Pemba, ili iweze kuzipangia mpango wa matengenezo yake kwa kila mwaka. Vile vile, Serikali kupitia Wizara ya Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ imeshaandaa andiko la mradi wa barabara za ndani zenye jumla ya urefu wa kilomita 250 na sasa limewasilishwa Tume ya Mipango kwa ajili ya kutafutiwa fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo.

**Mhe. Bakari Hamad Bakari:** Nakushukuru Mhe. Spika, kwanza naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini pamoja na majibu hayo naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Ujenzi wa barabara hii ni muhimu sana na umuhimu wake umekuja kutokana na kumuenzi pia Kiongozi Dkt. Omar Ali Juma kwa sababu barabara hii imepita kwenye kaburi lake lakini pia imepitia kwenye Skuli ya Dkt. Omar Ali Juma.

a) Je, ni juhudi zipi, Wizara yako au Mhe. Waziri umefanya kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa haswa kwa kushirikiana na Jamhuri ya Muungano ukizingatia kwamba kiongozi huyo alikuwa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri wa Tanzania.

**Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika naomba nijibu swali la nyongeza la Mhe. Bakari Hamad Bakari kama ifuatavyo. Kwanza nakubaliana na yeye kwamba barabara hii imekwenda katika kaburi la kiongozi wetu mstaafu ambaye alihudumu kwa heshima na taadhima kubwa kwa ajili ya nchi hii. Kama zilivyo barabara nyengine ambazo bahati nzuri kuna viongozi wetu wastaafu ambao wamekwenda kulazwa katika malazi ya kudumu. Tumhakikishie kwamba ushauri wake tumeupokea na tutashirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na ushauri wake wa kushirikiana na Wizara au kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuona namna ya kuwaenzi viongozi hawa kwa kuzifanyia ukarabati wa kutosha barabara hizi. *(Makofi)*

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Spika, kwanza nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kabla sijamuuliza swali langu Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwanza nataka kutoa pongezi kubwa sana kwa Timu ya Simba *Sports Club* kwa kuweza kuihakikishia dunia kwamba ni kweli Tanzania sasa imeshaingia kwenye Uchumi wa Kati na kwa sababu ya mpira uliochezwa jana ulikuwa ni mpira wa biriani ya mbuzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kuumuliza swali Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa majibu mazuri na nilikua naomba hili jibu alilolitoa alifanyie kazi hasa kwa kuzingatia kwamba marehemu kiongozi wetu Dkt. Omar Ali Juma kwamba aliitumikia nchi hii kwa moyo wake mkubwa na alikuwa ni msaada sana kwa jamii. Kwa hiyo, nafikiri ukiacha kile kiwango cha kifusi , ikitiwa lami barabara ile basi itakuwa ni vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Swali langu ni kwamba. Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ alivyokuwa akijibu alisema kwamba wanajaribu kuangalia barabara ile ya Wawi lakini pamoja na barabara nyengine za Zanzibar. Mimi swali langu lipo hapa, kwa upande wa wenzetu kule Tanzania bara, *Tanroad* wanashughulikia sana hizi barabara za ndani na ndio maana hata unapokwenda katika vijiji mbali mbali, kila baada ya mvua za masika ni TARURA.

Kila baada ya mvua za masika barabara zile utakuta zinatengenezwa katika kiwango cha kifusi lakini zinakaa kwa muda mrefu. Lakini kwa hapa kwetu, utaratibu huo haupo. Je, Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ atakuwa tayari kushirikiana au kwenda kujifunza au kushirikiana na wenzetu wa TARURA ili kubadilishana

uzoefu, ni namna gani wanavyotumia ili na sisi barabara zetu za ndani ziweze kuja kushugulikiwa. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hamza Hassan Juma swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza mashiriakiano yetu na TARURA tayari yapo. Hata barabara ambazo tumeanza kuzifanyia upembuzi yakinifu tumezifanya kwa kushirikiana na wenzetu wa TARURA. Kwa hivyo mashirikiano hayo tayari tunayo lakini la msingi tutayaongeza katika kufika malengo. Kwa kuongezea niseme kwamba ni lazima Waheshimiwa Wajumbe tuelezane hapa kwa sababu ndio sehemu yenyewe ya kuweza kuelezana hali halisi.

Kimsingi fedha ambayo hua inatengwa na serikali kwa ajili ya ukarabati wa barabara za ndani, ni fedha ambayo lazima tukiri kuwa ni fedha ndogo sana. Nasema hivyo kwa sababu ukitizama utaratibu wa ujenzi wa barabara za ndani huko tunakotoka, kila mwaka wa bajeti tulikuwa tukiidhinisha hapa kilomita zisizozidi tano na tunasema mwaka huu wa fedha Unguja, mwaka ujao wa Fedha Pemba.

Jambo ambalo ni lazima tukiri, si serikali bali na nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi ni vyema mkafahamu kwamba hiyo kwa upande mmoja ni changamoto. Tukubaliane sasa kwenye bajeti inayofuata ya mwaka 2021-2022 ikiwa bado jukumu hili litaendelea kusimmaiwa na Wizara ya Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ipo haja ya kuongeza mafungu haya.

Mhe. Spika, kwenye mafungu haya sisi serikali tupo tayari lakini Waheshimiwa Wawakilishi nyinyi ndio mtakua na mchango zaidi wakati tukipitisha bajeti hii kwa ajili ya kuiwezesha serikali kuweza kuwa na nguvu katika Ofisi hii ili kuzijenga barabara hizo za ndani. Kwa hivyo, nilitaka nitoe hilo ili tufahamiane tu kwa maana ya kuwa utaratibu wa sasa ukoje na uhalisia ukoje. Tumejiridhisha kwamba mara nyingi Waheshimiwa Wawakilishi wamekua wakiuliza barabara za ndani ni hizi tu, bado kilomita hizi.

Mhe. Spika, utaratibu ni kilomita tano kwa mwaka kwa fedha na tunafanya mwaka huu wa fedha Unguja, mwaka huu Pemba. Mwaka huu tuna barabara tatu Hawaii, Jango'mbe na Mwachealale. Ahsante.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kuniona. Mhe. Waziri wakati anaelezea alikua anaelezea changamoto ambazo zipo na *definitely* yeye ni mmoja wa serikali, anapoelezea hiyo changamoto na sisi wawakilishi ni wajibu wetu kusema barabara hii ijengwe na ile ijengwe na nyengine ujengwe kwa hivyo huo ndio wajibu wetu sisi. Sasa kama serikali imeona utaratibu huu unachangamoto huu wa sasa hivi una changamoto na sisi tunataka barabara za ndani zejengwe. Wewe kama serikali una mawazo gani mbadala ya kuhakikisha kwamba tunakwenda katika *effective procedures* zaidi kuliko ilivyo sasa hivi ya kujenga hizo barabara za ndani.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Saada Mkuya swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Nimesema kwenye jibu langu la msingi linalotokana na maswali haya ya nyongeza kwamba, kwa sababu tunajua kuna changamoto hiyo kama serikali, tumefanya upembuzi yakinifu kujua barabara zipi ndani ya Unguja na ndani ya Pemba ni barabara mbovu kwa sasa tumeshafanya upembuzi yakinifu kwa zaidi ya kilomita 200 na kitu. Tunachokifanya sasa ni kuandika na tumeshaandika andiko kupeleka Tume ya Mipango ili kutafuta ufadhili wa barabara hizo za ndani kupitia namna nyengine.

**Nam. 91**

**Changamoto Kuvuja Kwa Baadhi Ya Majengo Ya Skuli**

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis -** Aliuliza:-

Ili wanafunzi wapate elimu na kujenga ufaulu mzuri ni lazima hatua za maandalizi na msingi zipatiwe msukumo wa pekee ikiwemo usalama wa majengo. Skuli ya msingi ya Shumba Mjini na Maziwang'ombe zinavuja kupita kiasi.

Je, ni hatua gani Serikali itachukua kunusuru hali hiyo kabla ya msimu wa mvua kuchanganya.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ -** Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 91 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mwakilishi kwamba ili wanafunzi wapate elimu na kujenga ufaulu mzuri ni lazima hatua za maandalizi na msingi zipatiwe msukumo wa pekee ikiwemo usalama wa majengo. Skuli ya msingi ya Shumba Mjini na Maziwa Ng'ombe zinavuja kupita kiasi. Kuvuja kwa skuli hizo kunatokana na kuoza kwa mabati kwenye maeneo ya viungio. Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imeanza kuchukua hatua za kunusuru hali hiyo kwa kukutana na Kamati ya Maendeleo ya Jimbo la Micheweni ambapo imekubaliana kuwa majengo hayo ya skuli kuyaezeka upya kupitia fedha za Mifuko ya Maendeleo ya Jimbo mara tu zitakapoingizwa na kwamba Halmashauri nayo itachangia gharama hizo.

Aidha, Serikali chini ya uongozi wa Dk. Hussein Ali Mwinyi imeahidi na itatekeleza ahadi ya kuzifanyia ukarabati skuli zote za zamani (kongwe) hatua kwa hatua kutegemea na hali ya kiuchumi itakavyoruhusu.

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis:** Ahsante Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri kwanza nikupongeze kwa ufuatiliaji wako wa skuli hizi pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni lakini nataka nikwambie Mhe. Waziri lazima uwe makini, kwa sababu kama tunavyojuwa unaweza kuandikiwa tu kama skuli hii iko hivi na hivi mpaka mwenyewe ufuatilie je ulifuatilia lini na ulikwenda kufanya utafiti lini kuziona skuli hizo kama zinavuja maeneo yote ambayo ya mapaa na mikingo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Bihindi Hamad Khamis swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kimsingi ni kwamba kufuatilia tumefuatilia na tumejiridhisha hiyo hali ambayo tumeieleza kwamba skuli hizi zinavujana zaidi katika maeneo hayo ya viungio nimuhakikishie kwamba umakini utaongezeka kuhakikisha kwamba tunachokuja kukisema ndio kile amabcho tumekwenda kukifanyia utafiti.

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mwanana na mazuri. Pamoja na majibu hayo naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa swali la msingi lilikua linahusiana na usalama wa wanafunzi hasa katika skuli za msingi kwa hiyo naomba kuchukuwa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri katika skuli yetu ya Ndijani ya msingi kuna jengo la asili ambalo limeangukiwa na msufi takribani miaka miwili nyuma na jumla yalikuwa mabanda matatu, mabanda mawili tayari tumejenga Mbunge na Mwakilishi na wanafunzi wanaendelea kupata huduma. Je wizara yako inachukua hatua gani kwenda kulihami jengo ambalo limebakia la tatu ili kunusuru maisha ya wanafunzi lakini pia kuihami skuli ile ya kihistoria isipoteze uhalisia wake.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Issa Haji Ussi mwakilishi wa wananchi jimbo la Chwaka swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Nimueleze Mhe. Mwakilishi kwamba serikali itachukuwa jitihada ya kuinusuru skuli hiyo ya kihistoria lakini katika kulifanya hilo pia nimuhakikishie kwamba tutawenda kuiona skuli hiyo hali yake ilivyo ili sasa tuweze kujiridhisha na tathmini halisi ya kuweza kuinusuru skuli hiyo ya Ndijani.

**Mhe. Miraji Khamis Mussa:** Nikushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi lakini nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri yanayoleta matumaini katika kuwatumikia wananchi. Mhe. Waziri pale Chumbuni kuna skuli ya Msingi ya Mwembemakumbi ambayo ni skuli ya kihistoria kama ilivyo ya Ndijani maana ilijengwa kabla ya Mapinduzi. Inavuja na inahitaji ukarabati mkubwa, je ni lini serikali itaifanyia ukarabati skuli hiyo.

Pili,kwa kuwa ni jengo la kihistoria na linajulikana kote kama kukarabati serikali itashindwa ni lini serikali au wizara yako itakaa na Wizara ya Utalii kuliingiza katika makumbusho ili tupate tija kwa njia nyengine.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Samahani Mhe. Spika, hili swali la pili naomba Mhe. Miraji Khamis alirudie.

**Mhe. Miraji Khamis Mussa:** Mhe. Spika, namwambia tu Mhe. Waziri kwa kuwa skuli hii ni ya kihistoria, na kwa kuwa ilijengwa kabla ya hata Mapinduzi. Sasa wizara yako pengine inaweza kushirikiana na Wizara ya Utalii kama imeshindikana, kule mwanzo lini utaijenga, lakini kama imeshindikana maana tuipeleke kwenye hatua ya gofu ili tupate tija kwa njia nyengine.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa mwakilishi wa wananchi wa jimbo la Chumbuni swali lake la nyongeza lenye sehemu (a) na (b). Lini ukarabati utafanyika nimuhakikishe tu kwa maana hali ya fedha itakaporuhusu tutaweza kufanya ukarabati wa skuli yake hii au skuli yetu hii ya Chumbuni msingi. Swali lake la pili la kwamba sasa kama tumeshindwa tushirikiane na Wizara ya Utalii kwa maana ya kwamba ligeuke kuwa gofu, mimi nasema kwamba serikali bado haina mpango wa skuli ile kuifanya kuwa gofu. *(Makofi)*

Nimuhakikishie tu kwamba skuli ile serikali inaitambua uwepo wake na itaendelea kuifanyia ukarabati ili iendelee kutumika kwa matumizi ya kawaida na sio kuipeleka Wizara ya mambo ya Kale kuhesabika kwamba ni gofu.

**Nam. 28**

**Ucheleweshaji wa Vyeti vya Kumaliza Masomo**

**Mhe. Salma Mussa Bilal -** Aliuliza:-

Kumekuwa na ucheleweshaji wa kupatikana vyeti vya kumalizia masomo vya kidato cha Nne na Sita kwa wanafunzi baada ya kumaliza mitihani yao, jambo ambalo linawaletea usumbufu pale wanapotaka ama kuendelea na masomo au kuomba kazi kwa kutakiwa kupeleka cheti halisi na sio *"result slip"*.

Je, Wizara kwa kushikirikana na *NECTA,* ina mpango gani wa kuhakikisha vyeti hivyo vinapatikana kwa wakati ili kuwapunguzia usumbufu vijana wetu wanapomaliza masomo.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali -** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 28 kama hivi ifuatavyo:-

Kabla ya kujibu suali hili napenda kutoa maelezo machache kuhusu utaratibu wa *NECTA* kutoa vyeti vya wanafunzi wa Kidato cha nne na sita. Utaratibu uliopo ni kwamba mara matokeo ya wanafunzi yanapotolewa, *NECTA* hutoa *"Results slips"* ndani ya miezi mitatu ili kuwawezesha wanafunzi kutumia *Slips* hizo endapo ikitokea mwanafunzi anataka kuomba ajira au kujiunga na chuo kwa masomo zaidi. Kwa wanafunzi wa Kidato cha nne vyeti vyao huchukuwaa muda wa

mwaka mmoja ili kutoa nafasi kwa wanafunzi ambao wanataka kukata rufaa au kuhakiki taarifa zao za majina na alama za masomo walizowekewa. Aidha kwa wanafunzi wa Kidato cha sita vyeti vyao huchukuwa miezi sita katika matayarisho mpaka kutolewa.

Mhe. Spika, suala la kuchelewa kutolewa kwa vyeti hivyo ni kutokana na kufuata utaratibu huo uliowekwa na *NECTA* na mara tu vyeti hivyo vinapokamilika na kuwasilishwa katika Taasisi zetu, suala la ucheleweshwaji linakuwa halipo labda iwe mwanafunzi mwenyewe kajicheleweshaji kuchukuwa cheti chake kwa sababu zake binafsi. Bado tunasisitiza kuheshimu utaratibu wa *NECTA* ambao unalenga kuondoa usumbufu katika vyeti hivyo.

**Mhe. Spika:** Mhe. Salma Mussa Bilal swali la nyongeza.

**Mhe. Salma Mussa Bilal:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Katika jibu lake mama Mhe. Waziri alisema kwamba vyeti vya kidato cha nne vinachukuwa mwaka mmoja lakini kimsingi mwaka mmoja ni mwingi na ukizingatia kwamba wanakuwa wanapata shida wakati wanapoomba kwa kuambiwa kwamba *result slip* inakuwa hazitakiwi na wala hazitumiki na nataka kumuuliza Mhe. Waziri ni juhudi gani serikali itachukuwa kuona kwamba muda huu wa mwaka mmoja unapunguzwa na kuwekwa angalau mieizi sita au mitatu ili kuwaondolea usumbufu vijana wetu hawa.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Salma Mussa Bilal mwakilishi wa wananchi kutoka Mkoa wa Kusini kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, utaratibu huu ulivyoekwa ni kwamba umezingatia kwa pande zote mbili kwa upande wa *NECTA* upande wa Wizara ya Elimu lakini pia kwa upande wa wanafunzi au wananchi kwa ujumla. Suala la kuwekwa mwaka mmoja ni la msingi kwa sababu wakati mwengine inatokezea kama mwanafunzi panakuwa pana *error* pengine katika *spellings* au pengine anakata rufaa hakuna na taarifa zilizokuwemo. Kwa hiyo katika kipindi kile cha mpito kwa mfano hadi hivi sasa kwa mtihani wa *form four* tayari matokeo yashatoka wanafunzi hupatiwa zile *notification of results*. Sasa hizi ndio zinakuwa ni karatasi ambayo ataitumia pale katika maeneo kama ataenda kuomba kazi au atahitaji kujiendeleza kimasomo na hili halina tatizo lolote. Kwa sababu siku hizi kutokana na mazingira tulionayo unawasiliana tu kwa *proof* ukitaka kwa *NECTA* kwa sababu kila skuli inapewa namba yake ambayo ni *index number* katika skuli namba ya mwanafunzi kwa mfano skuli hii xy inaweza kuwa S120/namba ya mwanafunzi.

Kwa hiyo ukipeleka tu ile dakika moja unakuwa unajibiwa, kwa hiyo suala la kwamba hii sio changamoto iliokuwepo. Cha msingi ni kuhakikisha kwamba mwanafunzi anahakikisha zile taarifa zake ili anapokwenda kufuata cheti chake baada ya mwaka mmoja kwa upande wote basi anakuwa na taarifa zake sahihi. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri

naomba kumuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri alizungumza kuhusu suala la kukataliwa kwa *result slip.* Je Wizara yako imeshakaa na Wizara ya Elimu Tanzania Bara ili kuhakikisha kwamba vile vyuo vinavyotoa *order* ya mafunzo kwa mwaka au miaka na kuendelea kuweza kuzikubali *result slip* hizi ili kuona vijana wetu wanaweza kujiunga na vile vyuo ili kuendelea na masomo yao.

**Mhe. Spika:** Mhe. sijui kama unaweza kulijibu hili.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Naomba arudie.

**Mhe. Spika:** Hebu rudia kidogo.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Nasema hivi Mhe. Waziri, vijana wengi wanapotaka kujiunga kwenye vyuo iwe hapa Zanzibar au Tanzania Bara wakati Vyuo vinapotangaza masomo na vijana kutaka kwenda kujiunga na vile vyeti vinachelewa. Je, Wizara yako imeshakaa na Wizara ya Tanzania Bara ili kuhakikisha kwamba Vyuo vinawapokea hawa wenye *result slip.*

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama majibu nilivyotoa changamoto inakuwa haipo katika cheti au namba ya *result slip* ambayo ni *notification* yake ya mwanafunzi ya *results*. Changamoto inakuwepo katika herufi au jina kwa mfano jina la Mohammed unapomuandika 'u au o' au ukaikosa 'm' ina maana *system* nzima katika *computer* haitakuwepo au tarehe yake ya kuzaliwa ukiongeza ukibadilisha baada ya mwezi wa tatu ukamwandika mwezi wa nne, ina maana taarifa za yule mwanafunzi zinakuwa sizo. Cha msingi ni kwamba kila mwanafunzi baada ya kupokea *results slip* yake anatakiwa ahakiki taarifa zake ili sasa cheti chake kinapotoka kinapokwenda katika vyuo kule kunakuwa hakuna matatizo yoyote, cha msingi kila kitu kinakuwa kinakwenda vizuri, na hivi hasa zaidi katika *vocational training* kwa sababu hawa ambao wanataka kwenda vyuo kutoka kutoka *four* inakuwa muda wao bado kwa sababu inabidi waanze tena katika kuchukua *diploma* lakini zaidi kwa hawa ambao ni *A-Level* muda wao unakuwa ni muafaka katika kuendelea na masomo. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Nam. 36**

**Kupatiwa Stahiki Ya Posho La Likizo Kwa Wakati Kwa Wafanyakazi Wanaokwenda Likizo**

**Mhe. Hassan Hamad Omar** – Aliuliza:-

Ni haki ya mfanyakazi kupata mapumziko/ likizo kila mwaka mara moja au baada ya zaidi ya mwaka na anastahiki pia kupata posho la kujikimu wakati akiwa mapumziko.

(a) Kwanini Wizara imekuwa na usumbufu wa kutoa posho kwa wakati huku ikijua kwamba posho ni haki ya wafanyakazi.

(b) Je, utawasaidiaje wafanyakazi walionyimwa au kucheleweshwa kupewa posho zao wakiwa likizo.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali –** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 36 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Napenda tuelewe kuwa ulipaji wa posho za likizo hutegemea upatikanaji wa fedha zinazotokana na matumizi mengineyo (OC). Wizara hupokea fedha kutoka Serikali Kuu kulingana na mgao wa fedha hizo kama ilivyopangwa. Miongoni mwa matumizi ya fedha hizo hupatiwa walimu na wafanyakazi wengine wanaodai maposho yao. Ninapenda kutoa taarifa kwamba kwa mwaka 2020 hakuna mfanyakazi anayedai posho lake la likizo. Kwa sasa Wizara ipo katika matayarisho ya ulipaji wa maposho kwa wafanyakazi wanaodai kwa mwaka 2021.

(b) Hakuna mfanyakazi aliyenyimwa posho, wala Wizara haina dhamira hiyo. Ucheleweshaji wa kulipa posho ikiwa utatokea unatokana na kuchelewa kuingia fedha kutoka Serikali Kuu.

**Mhe. Hassan Hamad Omar:** Nashukuru. Mhe. Waziri nakushuru kwa majibu yako mazuri lakini pamoja na yote hayo naomba nikuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri kwa kuwa sisi ni wawakilishi wa wananchi na hapa tunawasemea wananchi na haya yanayotoka miongoni mwao yanatoka kwa wananchi. Je umetwambia kama hakuna mfanyakazi anaedai posho lake la likizo. Mhe. Waziri nakuuliza sasa ikitokezea mwananchi au wananchi wakajitokeza kuwa wanadai upo tayari kupokea malalamiko hayo na kuwafanyia haki zao.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Hassan Hamad Omar mwakilishi wa wawanchi kutoka jimbo la Kojani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, serikali ina majukumu ya kuwahudumia wananchi na katika kuwahudumia wananchi lazima tupo wengi kasoro zitatokezea na Wizara ya Elimu sisi Mhe. Spika, tuna wafanyakazi zaidi ya elfu tisa kwa ujumla na bado tuna malengo ya kuajiri wafanyakazi zaidi. Katika utaratibu ambao tunaokwenda nao ikiwa kwenye walimu pamoja na suala zima la ugatuzi inawezekana naomba nifahamike. Inawezekana katika kazi zetu na utaratibu wa kulipa hizi stahiki za walimu wetu pengine kuna mwalimu au mtumishi mmoja atakuwa yeye jambo lake halijakaa sawa. Sisi kwa upande wa serikali hatuna malengo hayo ya kumdhukumu mtu lakini kuhakikish akwamba utaratibu wa kisheria. Mhe. Spika, mimi niwaambie Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wako watu wanadai pengine inawezekana hata katika changamoto zinatokea tunawasikiliza na kuwafuatilia kwa hiyo suala lako hili Mhe. Mwakilishi sisi tupo tayari kukaa na wewe pamoja na hao wahusika ili tuweze kuwasaidia na kuhakikisha kwamba tatizo lao tunaliondosha na kama serikali tunalichukuwa na kulifanyia kazi, ahsante sana Mhe. Spika.

**Nam. 88**

**Ujenzi Wa Ukuta Katika Chuo Cha Kiislamu Micheweni**

**Mhe. Shamata Shaame Khamis -** Aliuliza:-

Licha ya Serikali kufanya juhudi kubwa ya kuendeleza ujenzi wa ukuta wa Chuo cha Kiislamu (CCK) Micheweni bado kazi hiyo haijakamilika na huku kuripotiwa vitendo vya uharibifu wa miundombini ya majengo na mali za wanafunzi ikiwemo wizi.

(a) Je, ni sababu gani zinazopelekea kazi za ujenzi huo kutokamilika mpaka leo.
(b) Je, tokea kuanza kwa ujenzi mpaka kufikia hatua ya ukuta ni kiasi gani cha fedha kilichotumika na kiasi cha fedha kilichobakia cha ukamilishaji.

(c) Je, ni muda gani Serikali ilikusudia kukamilisha ujenzi huo.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali –** Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 88 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

a) Shughuli za ujenzi wa uzio wa Chuo cha Kiislam yaani CCK Micheweni zilianza tokea mwaka 2013 hata hivyo kwa sasa ujenzi huo umesimama kutokana na changamoto za kutoelewana kati ya Serikali na wananchi waliokuwa wakitumia eneo ambalo uzio unatakiwa kupita, ambao tayari wananchi hao walishalipwa fidia ya mazao yao. Malalamiko yao ni kwamba hawana eneo jengine la kuendesha shughuli zao za kilimo, kwa sasa Serikali ya Wilaya ya Micheweni inafanya mazungumzo ya kutafuta muafaka na wananchi hao. Hivyo mara tu baada ya muafaka kupatikana Wizara yetu itakamilisha ujenzi huo. Aidha mwaka 2018/2019 tulitumia matofali ya ujenzi huo kwa uzio kujengea madarasa sita kutokana na uhaba mkubwa wa vyumba vya kusomea uliokuwepo chuoni hapo.

b) Ujenzi wa uzio huo ulipangwa kujengwa kwa awamu mbali mbali kufuatia upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida yaani *(OC)* Makisio yaliyopangwa kwa ujenzi huo hadi kukamilika kwake ni milioni 450 ambapo mita 650 zimeshajengwa kwa hatua ya awali bado plasta na rangi, kati ya mita 1400 za uzio huo jumla ya Shilingi milioni 70,399,300/= zimeshatumika na hadi kukamilika kwake kiasi cha Tshs. 379,600,700/ zinahitajika.

c) Awali ujenzi ulitarajiwa kukamilika kabla ya mwaka 2020 lakini umesimama kutokana na changamoto tulizozipata tulizoainisha hapo awali, ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mhe. Spika, naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa kujibu maswali vizuri, lakini nataka kuuliza maswali madogo ya nyongeza (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kupitia mazungumzo hayo ambayo ameyazungumza Mhe. Waziri ni lini wananchi tutegemee kwamba ufumbuzi utapatikana ili kazi hiyo iweze kuendelea kama vile ambavyo Serikali imepanga.

b) Ardhi tunajua kwamba ni mali ya Serikali kama kweli kuna tatizo hilo kuna ugumu gani wananchi wa maeneo hayo kupatiwa maeneo mengine kama vile ambavyo tumekuwa tukishuhudia wananchi wengine wanapatiwa maeneo.

c) Kuna tuhuma kwamba wananchi hawajachukua fidia lakini kama wamechukua fidia nilitaka kujua majina ya wananchi ambao wamepewa fidia na fedha ambazo zimelipwa kwa ajili ya fidia hizo.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri maswali mawili tu (a) na (b) ndio ujibu.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, sisi kwa upande wa Serikali malengo yetu ni kuhakikisha kwamba katika eneo husika wananchi wanafaidika na suala hili tunakuwa tunakwenda nalo muda mrefu, hadi miliki ya eneo hili imetolewa tokea tarehe 15/11/1998 na eneo lote hili kwa ukubwa wake ni *square miter* 1,020,000. Eneo ambalo hivi sasa kuna mgogoro ni dogo sana ni *Square mitere* 3,500 na nimuombe Mhe. Mwakilishi wa wananchi kwamba yeye akiwa kiongozi wa jamii ile ya watu ambao anawawakilisha, basi angalau asaidie pia kushiriki vikao baina ya Serikali zetu za Wilaya pamoja na wananchi ili kutafuta muafaka. Kwa sababu mwisho wa siku hichi chuo kinatumika sio kwa ajili ya wanafunzi wanaotoka maeneo tofauti lakini pia kwa wananchi katika eneo linalohusika. Kwa hivyo nimuombe tu kwamba hili jambo la msingi na sisi tutaendelea kwa upande wa Serikali kuweza kulisimamia kadri tutakavyokwenda katika siku.

Suala la wananchi katika fidia hili nafikiria Mhe. Spika, ulilioondoa yalikuwa mawili lakini kwa faida ya Mwakilishi nitampatia kwa maandishi ili ajue mwenyewe ni kiasi gani ambacho kimetolewa ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Waziri umesema kuwa ukuta umejengwa tangu 2013 ni kweli lakini pia unajua kwamba pale wapo wanafunzi wanawake na kama unavyojua sasa hivi kuna udhalilishaji mwingi, wewe huoni kama ipo haja ya kuweka walinzi au kuweka maeneo sahihi kuweza kuzuia wananchi na watu waovu kuingia pale kwenye maeneo ya skuli.

Lakini pia jengine Mhe. Waziri,kama tunavyojua chuo hichi kimeasisiwa mwaka 2001 huoni kama ni muda mrefu sana kuwa ukuta huu haujajengwa na kama ulivyoeleza kama kuna watu

waliokuwa hawajalipwa fidia, kwani hiyo mwanzo hawakulipwa fidia hawa watu ndio kiaanza kujengwa chuo hicho.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, suala la ulinzi katika chuo ni kitu cha lazima ulinzi upo, lakini katika hili eneo kama nilivyosema ni katika familia ambazo ziko tano ambazo tumekuwa nazo muda mrefu ambao wanadai katika viwanja vyao fidia. Kama nilivyosema mazungumza kati yetu na wananchi yanaendelea na sisi tunapopata fedha ambazo za kuweza kuboresha ukuta kama fedha ambazo tumeainisha katika jibu mama nilichokisema, ambazo hadi sasa tunatarajia kupokea au kupata katika miezi ya mbele ambazo ni milioni 370 ili tuweze kumalizia ukuta huo.

Mhe. Spika, cha msingi katika suala hili zima katika vyuo au maskuli sio kwa upande wa kaskazini kwa Chuo chetu cha *CCK* kwa upande wa Pemba, tuna changamoto katika maeneo mengi cha msingi ni kwamba kamati za elimu au skuli katika maeneo husika na wananchi pamoja na masheha ni kusimamia hizi skuli, kwani mwisho wa siku serikali imejenga kwa ajili ya wananchi na tunatambua hili suala la udhalilishaji kwa upande wa wanawake, cha msingi sisi kwa upande wa Serikali tumejitahidi kuimarisha na kuondosha hizi kasoro.Tuombe tu kama kuna taarifa zozote ambazo mnazo ambazo zinatia wasiwasi basi tuletewe tuweze kuzifanyia kazi. Hadi hivi sasa kwa upande wa Serikali hatujapata hizo taarifa lakini tutalichukua hilo kama uliviyosema ili kulifuatilia kwa undani. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Nam. 51**

**Utaratibu wa Ajira za Walinzi Katika Vibanda vya Maji Vilivyopo Chini ya Zawa**

**Mhe. Haji Shaaban Waziri** – Aliuliza:

Mamlaka ya Maji Zanzibar imekuwa na utaratibu wa kuwaweka walinzi katika vibanda vya maji kwa ajili ya kuvilinda vibanda hivyo, hata hivyo, kwa kuwa kazi za ulinzi ni ya kudumu lakini wanaofanya kazi hizo wameweka sawa na wafanyakazi wa kujitolea na kuwapatia posho kwa ajili ya kazi hiyo.

Je, Mamlaka imeandaa mpango gani wa kuwaajiri walinzi hao ambao wameshafanya kazi kwa miaka mingi hadi sasa.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini** - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 51 kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, vituo vya maji viliopo ni 316 ambapo kwa Unguja ni 187 na Pemba ni 129 ambapo kila kituo kinahitaji walinzi watatu ambao watapishana kwa mgawanyo wa masaa nane kila mmoja na kwa kuwa, vituo vya maji ni vingi hivyo inahitajika jumla ya walinzi 948.

Aidha, kutokana na idadi hiyo kuwa kubwa katika kukidhi mahitaji ya walinzi kwenye vianzio vya maji na kwa kuwa Mamlaka ya Maji haina uwezo kwa sasa kukidhi gharama za ulinzi uajiri wa walinzi wa vituo kama ilivyoonesha idadi inayoeleza hapo juu.

Hivyo, Mamlaka ya Maji katika kipindi hiki, ina mpango wa kuendelea na walinzi hao kwa mkataba na uwezo ukiruhusu tutaajiri kulingana na mahitaji ya maneneo hayo.

**Mhe. Haji Shaaban Waziri:** Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Sheria ya Utumishi Na.2 ya mwaka 2011 kwenye ajira ya kudumu inatutaka tusiajiri watu kwa mkataba bali kwa kuwa kazi hiyo ya kudumu waajiriwe kwa mkataba wa kudumu na kwa kuwa tuna wafanyakazi wengine wamefika kufanya kazi miaka kumi hadi leo na wengine zaidi ya hapo.

Je, lini sasa Serikali itawaajiri kwa mkataba wa kudumu ili na wao wapate haki zao.
**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kama ambavyo nimeeleza katika jibu mama vituo hivi ni vingi na hawa watu ni wengi jitihada ya serikali ni kuhakikisha kwamba watu hawa wanaajiriwa kadiri hali itakavyowezekana, tutafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba tunakwenda kulingana na masharti ya Sheria Na. 2 ya mwaka 2011 aliyoeleza Mhe. Mwakilishi, kwa hivyo kadiri hali itakavyoruhusu tutawaajiri hawa watu kwa kudumu ili kuondoa changamoto hii iliyokuwepo ya ajira ya mkataba.

**Mhe. Ussi Haji Ussi:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mhe. Spika, suala la walinzi katika vibanda vya maji nadhani tusilichukulie kwamba ni suala jepesi tu kwa sababu kinachozungumziwa hapa maana yake ni uhai wa Wazanzibari, uhai wa wananchi wetu akitokea mtu akenda aki-*contaminate* maji yale kwa maana kwamba waathirika ni watumizi wa maji yenyewe.

a) Je, Serikali imebadilisha maamuzi yale yaliyoamuliwa kwamba maeneo yote ya uzalishaji wa maji yalindwe na vikosi vya SMZ kwa kuzingatia tu usalama wa maeneo yenyewe, mifano ilianza eneo la Mnara wa Mbao na baadhi ya matangi ya mjini. Je, serikali imebadilisha uamuzi.

b) Suala langu la pili hawa ambao wameajiriwa kwa mikataba na kama maelezo ya Mhe. Waziri kinachokimbiwa hapa ni gharama, hawa wanaoajiriwa kwa mikataba je, hawalipwi na kama wanalipwa utaratibu wao uko je.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Suala la kutumia vikosi bado lipo utaratibu unaendelea ila hatujafikia pahala muafaka kwenye hili lakini tutakapokamilisha taratibu tutakuja na jawabu muafaka kwamba sasa tunatumia walinzi wa vikosi vya SMZ badala ya hawa wengine.

Mhe. Suala la walinzi waliopo wanalipwa lakini malipo yao ni posho za kawaida hasana mshahara kamili.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri visima vingi havina walinzi na sisi wengine tumeshanyanyua mikono walinzi wetu ni mungu tu inatosha, kisima cha Ndagoni tangu mwaka 2016 na alikwenda Naibu Katibu Mkuu wa *CCM* Dkt. Mabodi kukizindua na akasema kituo kile kiwekewe uzio angalau pale watu wasifunge ng'ombe.

Je, ni lini sasa kisima kile ama kimekosa mlinzi huu uzio lini utakwenda kuwekwa pale ili kuhakikisha kuwa kisima kile kinakuwa salama.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwanza naomba nikiri kwamba visima vingi havina walinzi na visima vingi havina uzio jitihada tunayokwenda nayo ni kuhakikisha kwanza visima vyote tunaviwekea uzio pamoja na kujenga vibanda ili kuviweka katika mazingira ya usalama zaidi, kisima cha Ndagoni ni miongoni mwa kisima ambacho kimo kwenye utaratibu wa kuwekewa uzio pamoja na kibanda.

**Nam. 63**

**Ucheleweshwaji wa Fidia kwa Wananchi Walioathirika na Ujenzi wa Barabara**

**Mh. Habib Ali Mohamed** - Aliuliza:

Naipongeza Wizara kwa kufanya kazi nyingi sana za ujenzi wa barabara.

(a) Je, ni sababu gani zilizopelekea barabara ya Wete- Gando na Wete – Konde kupata athari kabla ya kufunguliwa rasmi.

(b) Je, ni sababu zipi zilizopelekea watu waliostahiki kulipwa fidia kutokana na uharibifu wa nyumba zao uliotokana na ujenzi wa barabara hizo kutokulipwa stahiki zao.

(c) Je, ni sababu gani zilizopelekea kushindikana kwa ujenzi wa barabara kongwe ya Wete-Chake kupitia Piki.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi –** Alijibu:
Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 63 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ujenzi wa barabara ya Wete-Gando na Wete-Konde ulianza mwaka 2009 na kukamilika mwaka 2015. Barabara hizi zilipata athari mwaka 2017 ambapo katika kipindi hicho Zanzibar ilipata mvua kubwa ambazo hazikuwahi kunyesha kwa takriban miaka 40. Mvua hizo hazikuathiri barabara hiyo tu, bali ziliathiri maeneo kadhaa kama vile barabara ya Mtambwe katika eneo la Kisalani, Mkoani – Chake katika eneo la Changaweni na Mungu yupo.

(b) Mhe. Spika, Wizara imeweka utaratibu mzuri kabisa wa kuwalipa fidia wananchi ambao wanaathirika na ujenzi wakati wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara inapoanza. Aidha, katika mradi huo wananchi wote walioathirika kutokana na kupisha ujenzi wa barabara walifanyiwa tathmini na kuwalipwa fidia zao kabla ya ujenzi kuanza. Hata hivyo, mara baada ya ujenzi kukamilika kumejitokeza baadhi ya malalamiko ya wananchi ambao wamepata athari katika majengo yao kutokana na ujenzi huo. Hivyo, Malalamiko hayo tayari tumeshayapokea na tunaendelea kuyafanyia kazi.

(c) Mhe. Spika, kwanza naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mwakilishi kuwa Serikali haijashindwa kuijenga barabara ya Wete – Chake kupitia Piki, bali kilichotokea ni kwamba barabara hii fedha zake zilichelewa kupatikana kutokana na kasoro za Mkataba wa Mkopo baina ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na *SAUDI FUND.* Hata hivyo, kasoro hizo zimeshatatuka na kazi ya ujenzi wa barabara hiyo utaanza ndani ya mwaka huu wa fedha wa 2020/2021.

**Mhe. Habibu Ali Mohammed:** Nashukuru Mhe. Spika, kwa kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri napenda nimuulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa barabara ya njia Kongwe Wete/Chake kwa kupitia Piki imeshafanyiwa tathmini kwa kipindi kirefu sasa na bei za vifaa zimeongezeka, saruji imeongezeka bei, nondo imeongezeka bei na viwanja vimepanda bei. Je, Serikali ina mpango wowote wa kwenda kurudia tathmini ili wananchi wale wasijekuwa na malalamiko baadae.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Nilisema kwamba Serikali imeweka utaratibu mzuri wa kuwalipa fidia na tumeandaa utaratibu wa ku-*review,* utaratibu wetu ambao ulikuwa unatumika kwenye fidia na nilisema kwamba tayari tumeshakaa na Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ili tuwashirikishe kusaidiana katika shughuli hizo, kwa hivyo tutawalipa kutokana na hiyo *review* ambayo itakuwa inafanyika ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Mariam Thani Juma:** Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, nasikitika sana kwa majibu haya aliyoyatoa Mhe. Waziri, kwenye majibu yake amesema wananchi wote walioathirika kutokana na kupitisha ujenzi wa barabara walifanyiwa tathmini na kulipwa fidia zao kabla ya ujenzi kuanza, lakini Mhe. Spika, nina ushahidi kuna watu ambao walifanyiwa tathmini na hawakulipwa fidia zao.

a) Je, Mhe. Waziri pindipo kama kuna wananchi walioharibiwa vipando vyao na walitathminiwa na hawakulipwa fidia zao, wananchi hao ni zaidi ya kumi Mhe. Spika, je Mhe. Waziri utakuwa tayari kuwajibika na watendaji wako.

b) Kama huko tayari kuwajibika ni ipi kauli ya Serikali katika hatua ya kuwalipa fidia na stahiki zao kwa sababu nina uhakika na jambo ambalo ninalizungumza. Je, uko tayari kuleta orodha ya waliotathminiwa na waliolipwa kwa sababu katika jibu lako umesema kwamba malalamiko haya tayari tumeshayapokea na tunaendelea kuyafanyia kazi, Je, uko tayari kutuletea orodha ya hayo malalamiko uliyoletewa.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa naomba hili la kuwajibika sijui unakusudia kitu gani kuwajibika ajiuzulu au vipi, hapana hilo usilijibu jibu hili la pili Mheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

**Mhe. Spika:** Samahani kidogo Mhe. Waziri, Mhe. Maryam Thani liweke vizuri hili suala.

**Mhe. Maryam Thani Juma:** Mhe. Spika, kwa sababu hili jambo hata juzi tu walikuja watendaji wake sasa yeye nimesema yuko tayari kuwajibika kama hili jambo ni uongo yeye atatwambia.

**Mhe. Spika:** Mhe. Maryam Thani Juma Mhe. Waziri kaja jana tu hapa haya matatizo yapo tokea kile kipindi kilichopita *(Kicheko).*

**Mhe. Maryam Thani Juma:** Mhe. Spika, tokea hapo nilishamwambia kwamba kuna moja mbili tatu Mhe. Spika,

**Mhe. Spika:** Usitake kumbebesha huu mzigo hilo naomba nilichukue mimi la kuwajibika Mhe. naomba ujibu lile la pili.

**Mhe. Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, ahsante naomba kumjibu suala lake la nyongeza Mhe. Maryam Thani Juma kama ifuatavyo:

Katika swali langu nilipokuwa nalijibu la pili nilisema kuna wengine tayari wamelipwa nikasema hata hivyo, mara baada ya ujenzi kukamilika kujitokeza baadhi ya malalamiko ya wananchi kwa hivyo yakitokeza sisi tunayopokea na mimi tangu nilipokuja katika wizara sifiki hata siku tatu nayapokea yale malalamiko kwa hivyo tunayopokea tunayafanyia tathmini, ili tuangalie kiasi gani atalipwa, nani anastahiki kulipwa na kitu gani ambacho kitachokuwa kinastahiki kufanyiwa kazi.

Kwa hivyo yote hayo sisi tunayafanyia kazi wala hatuna tatizo na hilo na nilikiri kwamba katika wizara yangu jambo lenye mateso makubwa ni jambo la fidia na hilo kwa kweli tushirikirane kwa pamoja lina matatizo kabisa, kwa sababu saa nyengine anaweza akaletwa mtu ukahisi ile fidia yake haina mashiko sana lakini huwa anatetewa kwa hivyo pia naomba tushirikiane kwa suala hili, kwa sababu suala hili ni tatizo kubwa sana katika wizara yangu ahsante Mheshimiwa Spika.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri kwenye jambo hili umsaidie sana Mhe. Maryam Thani Juma maana yake kipindi kilichopita hapa alilia machozi humu Barazani kwa jambo hilo. Kwa hiyo anaponyanyuka kwamba uwajilibike najua ule uchungu wake unatokea wapi. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi** Mhe. Spika, ahsante nashukuru lakini tayari Mhe. Maryam Thani Juma tumekutana pembeni kule akanifahamaisha lakini nashangaa sasa hivi..

**Mhe. Spika:** Shirikianeni umsaidie sana mheshimiwa.

**Nam. 71**

**Mchakato wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege – Pemba**

**Mhe. Bakari Hamad Bakari -** Aliuliza:

Mchakato wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba umefanyika miaka mingi iliyopita, ambapo katika mchakato huo wananchi ambao wameonekana kuingia katika eneo linalokusudiwa kuwa ni sehemu ya uwanja huo walifanyiwa tathmini ya nyumba pamoja na vipando vyao.

a) Je, ni lini Uwanja huo unatarajiwa kujengwa.

b) Je, ni lini Serikali itawalipa fidia wananchi waliokwisha kufanyiwa tathmini ambao wameonekana kuwa ni waathirika katika eneo hilo la kiwanja.

c) Je, Serikali inatarajia kuwalipa wananchi hao fidia kwa kuzingatia thamani ile ya awali au kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha.

**Mhe. Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi -** Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suala lake Nam. 71 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekamilisha kazi ya Upembuzi Yakinifu wa ujenzi wa Uwanja wa ndege wa Pemba na tayari nyaraka hizo zimewasilishwa Wizara ya Fedha na

Mipango ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuombewa fedha za Ujenzi kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)*. Kwa hivyo, ni mategemeo yetu kwamba mara tu zitakapopatikana fedha hizo, kazi za Ujenzi zitaanza.

Mhe. Spika, hata hivyo katika suala hili serikali yetu ya awamu ya nane inaendelea kupokea wawekezaji walionesha nia ya kujenga na kuendesha uwanja huo. Kwa hivyo ikiwemo Oman na Uturuki kwa hivyo *ADB* wakija mwanzo tunakwenda nao wakija wengine Oman au Uturuki tutakubaliana naye kwa sababu wamekaa muda mrefu hatujui kinachoendelea.

Kwa hivyo serikali imeamua iendelee kupokea wawekezaji  ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Bakar Hamad Bakar:** Mhe. Spika, swali langu lilikuwa na (a), (b) na (c) majibu iliyopata ni majibu (a).

**Mhe. Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, nilikuwa naendelea samahani.

(b) Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kuanza kulipa fidia wananchi ambao wataathirika na ujenzi wa uwanja huo.

(c) Mhe. Spika, Wizara imeweka utaratibu mzuri kabisa wa kuwalipa fidia wananchi ambao wataathirika na mradi huo wa ujenzi. Hivyo, wananchi hao watalipwa kutokana na thamani ya fedha za sasa baada ya kufanya mapitio. Ahsante Mhe. Spika.

**Mhe. Bakar Hamad Bakar:** Mhe. Spika, nakushukuru kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini pamoja na majibu hayo mazuri naomba nimuulize swali moja lenye (a) na (b) la nyongeza kama ifuatavyo:

(a) Kwa kuwa ujenzi huu wa Uwanja wa Ndege mchakato wake umeanza muda mrefu nataka kufahamu ni vikwazo vipi ambavyo vilikwanza mpaka ujenzi huu mpaka leo haujaanza.

(b) Lakini jee tathmini hii kwa maana *revaluation of asset* ya wananchi kule itafanyika lini na lini watalipwa ukizingatia kwa majibu yako mama, amesema kwamba ni mwaka huu wa fedha 2020/2021 lakini hadi leo tathimini hii haijafanyika. Nakushukuru Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, ahsante naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Bakar Hamad Bakar kama ifuatavyo:

Hata sisi serikali tumeona inachelewa hii kazi na hizi pesa hazitoki kwetu fedha zinatoka kwenye mkopo wa bei nafuu wa Benki ya *ADB* nimesema mwanzo ambazo tunaomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pia tumeona kimya na ndio maana nikasema serikali pia imewalika wawekezaji kuhusiana na suala hilo kwa hivyo, ikija hiyo mwanzo tunawachukua lakini wakija wawekezaji tunaenda nao wawekezaji. Ahsante Mheshimiwa Spika.

**Mhe. Suleiman Makame Ali:** Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza.

Mhe. Waziri katika majibu yako umesema kwamba uwanja wa ndege Pemba mumeuombea fedha kupitia Benki ya Afrika, mumepeleka maombi kupitia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Serikali, lakini katika vipa umbele vya bajeti au vipa umbele vya serikali vinavyotaka kutelezwa uwanja wa ndege Pemba umo.

Sasa nikitaka kujua pamoja na fidia wananchi waanza kulalamika hivi sasa je, katika vipa umbele hivi inategemewa kwenye hiyo maombi mliyoomba kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au kuna mpango gani mwengine wa kuhakikisha kwamba vipa umbele hivi haviendi ile kwa miaka mitano, sita tunasubiri uwanja wa ndege wa Pemba.

**Mhe. Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, ahsante naomba kujibu Mhe. Suleiman Makame Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Hapa nirudie tu kwamba sisi pia tumeona *ADB* wanachelewa na ndio maana serikali imewaalika wawekezaji kwa sababu ya kipa umbele ambacho kipo wameona kuna umuhimu wake, tumeona serikali kuna umuhimu wa uwanja wa ndege wa Pemba kwa hivyo ni katika vipa umbele vyetu na tayari tumepokea wawekezaji kutoka Uturuki na Oman. Kwa hivyo tumeliona suala hili Mhe. Suleiman Makame Ali na tunalifanyia kazi. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Samahani kuna swali acha nimpe nafasi Mhe. Suleiman Haroub Suleiman

**Mhe. Suleiman Haroub Suleiman:** Mhe. Spika, ahasante pamoja na majibu mazuri ya serikali naomba kuuliza swali dogo sana kwa Mhe. Waziri.

Je, atakubaliaa na mimi kwamba kuna wananchi wanaoishi Shehia ya Chukwani kwa maana kwamba Chukwani/Buyu kupitia ujenzi wa uwanja wa ndege *terminal III* bado fidia zao hazijakamilika na wengine tayari washatangulia mbele ya haki.

Je, hawa waliobakia yuko tayari kuwalipwa fidia hiyo na kama pengine anatakanusha hilo je yuko tayari kuipokea orodha hiyo. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Mhe. Spika, ahsante naomba kujibu Mhe. Suleiman Haroub Suleiman swali lake la nyongeza narudia tu swali langu kwamba sisi tunaendelea kupokea hayo malalamiko ya fidia hata ya uwenja wa ndege wa *terminal III* pia nayo tunaendelea kuyapokea.

Kwa hivyo kama kuna wananchi bado hawajeleta tunaomba yaletwe wizarani kwetu tuyafanyie kazi ahsante mheshimiwa.

**Mhe. Spika:** Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu wa Baraza la Wawakilishi majibu ya ziada.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu wa Baraza la Wawakilishi:** Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Mhe. Waziri mimi naomba nieleze nitowe maneno ya ziada kama ifuatavyo:

Suala la fidia kwa *airport* ya Unguja nadhani zilitayarishwa orodha nyingi sana na kulikuwa na kamati maalum iliyowashirikisha wananchi wenyewe wakaazi wenyewe wa maeneo hayo na watu hao walilipwa fidia zao. Sasa jambo hili la fidia iwe Unguja iwe Pemba lazima tuwe na hadhari nalo sana, kwa sababu wengine hutumia ujanja humo ndani kwa hivyo ni suala ambalo linahitaji lihakikiwe vizuri sana. *(Makofi)*

Kwa sababu mara nyingi sana serikali inalipa, inakuja orodha nyengine inalipwa sasa hii kulipa lipa lazima ifikie mahala ifikie mwisho, sasa tuangalie hizo orodha ni za kweli kwa sababu hii *airport* ya Unguja watu walilipwa sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika unakumbuka kulikuwa na kamati iliyoshirikisha wananchi wenyewe sasa hawa wanashangaa wanakuja tena hapa na sawa sawa huko Pemba na Pemba kwenye barabara za Pemba orodha zilitayarishwa na hao ambao wako wanadai wanajulikana kama alivyosema Mhe. Waziri sasa tusije tukawa tunachukuwa orodha hapa tutakuwa hatumalizi malipo haya Mheshimiwa Spika.

**Nam. 5**

**Kukithiri kwa Vitendo vya Udhalilishaji Zanzibar**

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis –** Aliuliza:

Kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa ya vitendo vya udhalilishaji katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar, na kwa kuwa Serikali imeshatumia fedha nyingi kwa ajili ya kupunguza au kuondoa suala hili bila ya mafanikio.

Tukiachia semina na makongamano ambayo yamefanyika mengi bila ya kupata mafanikio, ni mikakati gani madhubuti ya Wizara iliyoandaliwa ya kuhakikisha vitendo hivyo vinaondoka.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny. Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto -** Alijibu:

Mhe. Spika, ahsante sana kabla sijamjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nilikuwa nitowe tu taarifa kwa Waheshimiwa Wawakilishi wafahamu kwamba katika majibu yale tunajibu ya Wizara ya Elimu siku hizi tunamwenendo kwamba tunahakikisha kwamba taasisi husika kila swali likijibiwa na wenyewe wanakuwepo na katika swali la leo la *CCK* Ofisa Mdhamini kutoka Pemba yuko na waratibu wa Wizara ya Elimu kwa hiyo ilikuwa muhimu tu Waheshimiwa Wawakilishi wafahamu.

Mhe. Spika, baada ya hapo naomba kumjibu swali namba 5 Mhe. Mwakilishi Mwantatu Mbarak Khamis kutoka Mkoa wa Kusini Unguja swali lake namba 5 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba ieleweke kwamba udhalilishaji ni suala mtambuka ambalo linahusisha Taasisi zote ziliopo katika jamii yetu katika uchangiaji, uondoaji au upigaji vita vitendo vya ukatili na udhalilishaji visitokee nchini mwetu, na kwamba suala hili si jukumu la Taasisi moja pekee, tunahitaji kushirikiana kwa pamoja katika kutokomeza vitendo hivyo bila kuoneana muhali katika ngazi zote za utekelezaji.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto itaendelea na jukumu la kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa kupambana na vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa mwaka 2017 hadi 2022. Mpango huu umeainisha majukumu na mikakati kwa kila Taasisi husika ili iweze kutekeleza majukumu hayo na kutoa taarifa za utekelezaji. Taarifa za utekelezaji zinatolewa kwa vyombo husika na hatua mbali mbali zinachukuliwa.

Mhe. Spika, kwa faida, mapambano yoyote yanahitaji gharama na sio fedha pekee katika kuondoa au kumaliza tatizo lililokuwepo. Kwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto miongoni mwa mambo ya msingi ni suala la kujitolea mtu binafsi, kutenga muda, kuimarisha vitendea kazi na fedha ili kukamilisha mahitaji ya kupambana na matendo hayo.

Mhe. Spika, mikutano, semina na makongamano yanayofanyika dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji yanasaidia kwa kiasi kikubwa katika:-

i. Kuhamasisha jamii na kujenga uelewa katika kujikinga na kutoa taarifa za matukio katika vyombo husika juu ya vitendo hivyo katika ngazi mbali mbali. Hadi sasa wananchi katika Shehia 150 (100 Unguja 50 Pemba) tayari wamefikiwa. Aidha, kupitia makongamano hayo, skuli ya msingi na sekondari Nungwi imejengewa ukuta; kuondoshwa kwa vichaka katika maeneo hatarishi; pamoja na kuondolewa kwa TV za nje katika baadhi ya maeneo;

ii. Kujenga uwezo kwa viongozi wa dini ili kuhamasisha jamii katika hotuba za sala za Ijumaa misikitini, mahubiri kanisani, madrassa na mikusanyika mengine ya kidini.

Mhe. Spika, Wizara pia, imetayarisha na kutekeleza mkakati wa mawasiliano na kupambana na vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa wanawake na watoto, imeimarisha mifumo ya Mawasiliano ya utoaji wa taarifa za matukio kwa watoto na vitendo vya Ukatili na Ushalilishaji wa Kijinsia kwa kupiga simu nambari 116 bila malipo yaani *(Free call);* pamoja na kufanya utafiti uliofanyika mwaka 2020 ukiwa na lengo la kujua ukubwa wa tatizo ili kuweka mikakati itakayosaidia kuondoa tatizo la matukio hayo.

Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii kuwaomba Wajumbe wa Baraza hili kuunga mkono mikakati hii na juhudi nyenginezo zinazochukuliwa na Wizara kwa makusudi katika kumaliza vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia katika ngazi zote.

Mhe. Spika, kuondoa udhalilishaji inawezekana tuanze Tuaanze na mimi na wewe, tafuta wengine watangulie. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis:** Mhe. Spika, ahsante nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali nyongeza, kwanza nichukuwe fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa juhudi kubwa aliyochukua ya kuanzia Mahakama ya Udhalilishaji, kwa kweli ilikuwa kiu ya wananchi walikuwa wakipiga kilele wakiomba na nimpongeza kwa hatua hiyo.

Lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu mazuri na ufasaha lakini nimuulize swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa vile sisi sote ni wadau wakupinga vitendo hivi au kupambana na vitendo hivi vya udhalilishaji na Mhe. Waziri alieleza kwamba kuna mikakati ya kitaifa ambayo taarifa zake zinatolewa katika vyombo husika.

Je, sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hatupaswi kuelewa mikakati hiyo na kama tunapaswa kuielewa naomba atueleze japo kwa uchache wake kwa faida ya wajumbe wa Baraza na wananchi kwa ujumla. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny. Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, suala la udhalilishaji ni kama nilivyosema katika maelezo ya mwanzo ni suala mtambuka linagusa maeneo mengi na kilio cha wananchi kwa ujumla na kwa sheria ambazo tunazosimamia sisi zinazotuongoza ni pamoja na Sheria Jinai namba 7 ya 2018, Sheria ya Ushahidi ya mwaka 2016, Sheria ya Mtoto namba 6 ya mwaka 2011 na katika mapambano haya mara nyingi hapa hata katika serikali ya awamu iliyopita au katika Baraza lililopita palikuwa pana ushauri mwingi ulitoka hapa juu ya katika mashine ya *DNA* kwa mfano na tayari hii mashine tayari imefungwa na inatumika. Lakini bado tunahitaji wananchi kusimamia katika utaratibu mzima kutoka tangu tukio linapotokezea mpaka ule ushahidi unapotaka kufikishwa ili katika vile vipimo vinavyotaka kufanyiwa viweze kufanyika kabla jalada halijaenda kupelekwa katika Ofisi ya *DPP*.

Sasa niseme tu katika mikati hii ambayo Mhe. Mwakilishi anayozungumza hivi leo kuwepo hapa sisi kulijadili na kuleta maelezo haya na serikali kuweza kujibu ni sehemu moja ya kuhakikisha Baraza linatambua mikakati hii, kwa hiyo Mhe. Mwakilishi alifahamu hili.

Lakini pia katika semina ambazo zote serikali na Kamati za Baraza la Wawakilishi zinapitia ni katika kufuatilia na serikali katika mshauri namba moja ni Baraza la Wawakilishi na kamati husika imekuwa inazungumza mara nyingi na Mhe. Spika, katika hata mkutano wa suala zima la udhalilishaji mimi nikuwepo na niipongeze sana Kamati yako ya Ustawi wa Jamii walikuwa na safari ya kwenda Makunduchi walikuja kushiriki katika mkutano ule na Mhe. Rais alikuwepo wakatambulishwa wote kamati na wakashiriki katika mkutano.

Sasa katika mikakati hii yote katika awamu hii ya nane hichi ndio kianzio chenyewe lakini cha msingi ni kwamba tuhakikishe kwamba katika wizara zote ndani ya serikali hii na taasisi, ni

kwamba katika yale mambo na maeneo ya wahusika serikali itajitahidi kwamba wawakilishi pamoja na kamati zako za Baraza tunashirikiana kwa pamoja kwa ujumla ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kwa kuniona ukanipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri miongoni mwa wanaokwamisha kesi hizi za udhalilishali ni baadhi ya madaktari ambao hawashiriki katika kutoa ushahidi.

Je, serikali ina mpango gani wa kukaa na madaktari kuwaeleza kwa kina kwamba inapokosekana ushahidi wao ni miongoni mwa kukwama kesi hizi zisiendelee.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny. Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto:** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Panya Ali Abdalla mwakilishi wa Kaskazini Unguja swali lake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza mimi sikubaliani naye kwamba madaktari wanaharibu ushahidi hilo sio kweli labla yeye kama anao uthibitisho wa kutuletea basi tutaungalia, lakini hilo jambo sio kweli. Madaktari wetu katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba ni wazalendo, wanafanya kazi kwa kujitahidi na katika suala hili zima la udhalilishaji wanachukizwa wao kwa sababu wao ni katika sehemu ambao wanaliona baada ya matendo kufanyika.

Labda Mhe. Mwakilishi nimkumbushie tu kwamba utaratibu wa suala la udhalilishaji kuna maeneo matatu.

Suala la kwanza panapotokeza unahitaji kuripoti katika tukio la ukatili katika kituo cha Polisi kilichopo karibu na huyo mtu ili kuanza uweze kupata *RB,* kisha unapatiwa *PF3* baada ya hapo inaonesha muathirika kwenda kituo cha mkono kwa mkono hasa kwa mtu ambaye ni mtoto na mtu mzima kwenda katika hospitali kwa ajili ya matibabu ya uchunguzi.

Lakini baada ya kumaliza hospitali anatakiwa mtu mhanga arudi tena polisi na katika mahojiano na upelelezi, baada ya hapo hatua itakayofuata hapo kama ni ripoti inakwenda kwa *DDP* na kasha kutengezewa jalada, ikiwa lile jadala halina mashaka yoyote *DPP* yeye anawasiliana na mahakama na endapo itatokeza kuwa mashitaka yote ya jalada haya yana matatizo basi taarifa za msingi inabidi ziimarishwe.

Hasa unakutwa sehemu ya daktari kama Mhe. Mwakilishi anapouliza ni sehemu moja ni mnyororo huu tangu tukio linavyofanyika. Kwa hiyo, mimi nimuombe tu Mhe. Mwakilishi kwamba utaratibu huu wazidi kutoa elimu hasa pale ambapo matokea yanapotokezea waweze kufuata utaratibu wa kisheria kama nilivyotaja mara ya mwanzo. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi kwa kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kabla ya kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri naomba nichukue fursa hii kuwapongeza sana *Simba Sports Club* na kuwatakia kheri katika safari ya mbele wanayoelekea.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Spika, katika majibu ya Mhe. Waziri amesema naomba nimnukuu. "Naomba ieleweke kwamba udhalilishaji ni suala mtambuka ambalo linahusisha taasisi zote zilizopo katika jamii yetu, katika uchangiaji, uondoaji au piga vita vitendo vya ukatili na udhalilishaji visitokee nchini mwetu, na kwamba suala hili si jukumu la taasisi moja pekee, tunahitaji kushirikiana kwa pamoja katika kutokomeza vitendo hivyo bila kuoneana muhali katika ngazi zote za utekelezaji".

Mhe. Spika, mara nyingi vitendo vya udhalilishaji vinapotokea tunaona mara nyingi wazee au wazazi wanahusika kwa njia moja au nyengine ama kushindwa kutoa ushahidi Mahakamani ama kumuozesha mume *victim*.

a) Je, ni lini serikali italeta sheria ya kumbana au kumtia hatiani mzazi yeyote atakayeshindwa kutoa ushahidi au kumuozesha mume *victim*.

b) Je, katika awamu hii ya nane miezi hii mitano je hali ya udhalilishaji ikoje, imeshuka au imepanda. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kaimu Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto):** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Shadya Mohamed Suleiman swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Mwakilishi kwa maswali yake mazuri, lakini katika kukumbushia mambo haya ambayo ni ya msingi juu ya suala zima la udhalilishaji. Mheshimiwa sheria zilizopo nilizitaja mwanzo kuna Sheria ya Mtoto, Sheria ya Mambo ya Jinai na mengineyo, lakini hili suala la kuja na sheria ya kumbana mzee kwa sababu utaratibu uliokuwepo ni utaratibu ambao unatumika sasa hivi kama una kasoro tutazidi kupata maoni kutoka kwa wadau.

Pia kama kunahitajika sheria serikali italizingatia hilo, lakini niseme tu kwamba tunapokuja leo na sheria ya kumbana Waziri itabidi tuje na sheria ya kuwabana walimu, itakuja baadae sheria ya kuwabana huko vyuoni kwenye madrasa, baadae itakuja sheria ya kuwabana pia wajomba katika familia. Sasa lazima tuangalie kwamba sheria tunapotunga, tunatunga sheria ili iweze kukidhi mahitaji katika maeneo yote, hatuwezi kutunga sheria kwa sababu ya mzazi tu. Tayari katika *universal declaration of human rights*, sheria zote za haki ya mtoto pamoja na wazee, vijana zote zimetajwa na sisi kama Tanzania ni wanachama na hili jambo linaeleweka. Kwa hiyo, mimi nimuombe Mhe. Mwakilishi mawazo yake pengine ni mazuri lakini pia inawezekana tufanye utafiti wa ndani kabisa ili tuweze kuangalia huo ushauri anaoutoa na yeye ni mzoefu katika masuala haya basi mimi nilichukue hili suala kwa upande wa wizara ili tuzidi kuangalia katika awamu hii.

Mhe. Spika, swali lake la (b) juu ya suala zima la utafiti kuangalia katika awamu hii ya Serikali ya Nane udhalilishaji je umepanda au umeshuka. Mhe. Spika, swali hili kidogo ni gumu kwa sababu jana pia viongozi wetu wametoa ripoti za kila mwezi, naomba tupate muda kidogo kama serikali halafu tufanye tathmini ya kiujumla kwa sababu mikakati yetu ambayo tunakwenda katika awamu ya nane inaweza ikatofautiana na ile mikakati ya awamu ya saba. Hilo

tutalichukua na uzoefu uliopatikana katika serikali ya awamu ya saba ili na sisi tuweze kupambana katika awamu ya nane, lakini kama nilivyosema mwanzo suala la udhalilishaji ni suala mtambuka kwa hiyo mapiganaji haya yanahitajika katika pande zote katika jamii. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Nam. 82**

**Kutokomeza Ugonjwa wa Malaria Zanzibar**

**Mhe. Azza Januar Joseph -** Aliuliza:

Serikali inastahili pongezi kwa kufanya jitihada kubwa ya kutokomeza malaria hapa Zanzibar kwa kutumia dawa ya kuuwa mbu wa malaria.

Je, kwa nini serikali isiweke mpango wa kuendeleza mradi ule kwa kuwa ulikuwa unasaidia kuuwa wadudu wengine ambao ni kero katika jamii kama mende, kunguni, chawa na hata inzi ambao husababisha maradhi ya mlipuko.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kaimu Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto)** - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 82 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kutokana na kushuka kwa maambukizi ya ugonjwa wa malaria kwa kiwango kikubwa kufikia chini ya asilimia moja tangu mwaka 2008, wizara ilishauriwa na Shirika la Afya la Dunia na washiriki wa maendeleo wengine kupiga dawa kwenye maeneo maalum yanayoendelea kutoa wagonjwa wengi.

Hata hivyo, kutokana na matumizi madogo ya vyandarua wizara imeona ni muhimu kuendelea kupiga dawa majumbani hata katika maeneo yanayotoa wagonjwa kidogo. Hatua hiyo itasaidia kuua wadudu wengine kama mende, kunguni, chawa na inzi ambao wanaleta kero katika jamii kama Mhe. Mwakilishi alivyogusia. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Azza Januar Joseph:** Ahsante Mhe. Spika, nashukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kulingana na majibu yake aliyotoa ni kwamba wizara itaendelea kupiga dawa majumbani hata maeneo ambayo yanatoa wagonjwa kidogo. Je, ni lini wizara itaamua kupiga dawa majumba yote ikiwa kero hii ya wadudu waharibifu kama kunguni inawasumbua sana wananchi hususan maeneo ya vijijini.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kaimu Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto):** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Azza Januar Joseph swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, swali la kupiga dawa majumbani au *fumigation* kwa ajili ya kupambana na vidudu ambavyo vina uharibifu kama kunguni, inzi ambao huja kutokana na mazingira ya joto, wakati wa matunda yakiwa mengi yanatumika ni suala la usafi, pia ni suala

ambalo na sisi kama wananchi tunatakiwa tuisaidie serikali, kwa sababu serikali haiwezi ikaingia kwa kila mtu nyumbani kwake mpaka jikoni kwake kumfanyia suala zima la usafi. Kwa hiyo, suala la kujikinga na usafi kwa wadudu wengine ni suala binafsi na nitoe rai katika suala hili kwa kuwapongeza sana wananchi kwenye maeneo tofauti hasa yale maeneo ambayo tulikuwa tunapata kero. Kwa mfano, magonjwa ya *cholera* na mengineyo.

Mhe. Spika, kwenye suala la wadudu kama wa *malaria*, wadudu hawa sisi tutaendelea kupiga dawa kadri pale uwezo unapoturuhusu, hadi jana wakati Mhe. Spika kama ulikuwa unapita hapa maeneo ya Mbweni, yapo maeneo korofi tulikuwa tunapiga dawa kwa ajili ya kupambana na malaria. Kwa hiyo, tuipongeze sana serikali tusijiangushe sisi wenyewe duniani sasa hivi Zanzibar tumesifiwa sana kwa kupambana na malaria. Lakini tunatakiwa tusilale tuendelee kupambana na niwaambie Waheshimiwa Wawakilishi *malaria* katika maeneo mengine hujitokeza na bado ipo. Kwa hiyo, mnapoona pale wananchi wetu kuna dalili za ugonjwa huo basi wafike katika vituo, lakini pia wataalamu wetu kufika katika maeneo husika kwenda kupambana na hao wadudu wa *mosquitoes*. Mhe. Spika kama unafahamu *malaria* wadudu wake hasa ni wanao-*cause* ni *plasmodium* kwa hiyo ni kwenda kuwafata hawa wadudu kupambana nao na yule *carrier* ambaye ni *female anopheles* basi tuweze kupambana na kummaliza. Ahsante sana Mhe. Spika.

**Mhe. Zawadi Amour Nassor:** Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii, miongoni mwa njia za kujikinga na *malaria* ni kulala kwa kutumia chandarua. Naomba nimuulize Mhe. Waziri kwa nini kumekuwa na changamoto kubwa katika Wizara yako ya Afya kugawa koponi za vyandarua kwa wananchi wetu.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kaimu Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto):** Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Zawadi Amour Nassor swali lake dogo na fupi lakini ni gumu la nyongeza. Mhe. Spika, swali hili itabidi nimjibu kwa maandishi. Ahsante sana.

**Mhe. Spika:** Ahsante waheshimiwa wakati wa maswali umekwisha na maswali yenyewe yamemalizika.

Waheshimiwa Wajumbe, nina matangazo tangazo la mwanzo nimeletewa na Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ambaye anawatangazia wajumbe wake wa Kamati ya Bajeti kwamba kutakuwa na kikao mara baada ya kipindi cha maswali na majibu katika ukumbi mkubwa. Kwa hiyo, anawaomba niwatangazie ili baada ya hapo wajumbe waweze kwenda kwenye kikao hicho.

Tangazo linalofuata pia ni tangazo la kuchukua fomu, Waheshimiwa Wajumbe mtakumbuka kuwa kwa mujibu wa ratiba ya mkutano wetu huu wa pili wa Baraza la Wawakilishi tutakuwa na uchaguzi wa viongozi wa jumuiya zetu tatu ambazo ni:

1. Jumuiya ya Wabunge wa Nchi za Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Parliamentary Association*) *CPA*

2. Jumuiya ya Wabunge Wanawake wa Nchi za Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Women Parliamentarians*) *CWP* na

3. Umoja wa Wawakilishi wa Kupambana na UKIMWI Zanzibar (UWAKUZA)

Kwa upande wa uchaguzi wa Jumuiya ya Wabunge wa Nchi za Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Parliamentary Association*) *CPA* na Jumuiya ya Wabunge Wanawake wa Nchi za Jumuiya ya Madola (*Commonwealth Women Parliamentarians*) *CWP* tawi la Zanzibar viongozi wafuatao watachaguliwa nao ni:

1. Mwenyekiti wa Kamati Tendaji wa Tawi
2. Makamu Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya Tawi
3. Wajumbe wengine watatu wa Kamati Tendaji ya Tawi na
4. Mweka Hazina wa Kamati Tendaji ya Tawi

Waheshimiwa Wajumbe, kwa uchaguzi wa Umoja wa Wawakilishi wa Kupambana na UKIMWI Zanzibar (UWAKUZA) viongozi wafuatao watachaguliwa nao ni:

1. Mwenyekiti
2. Makamu Mwenyekiti
3. Mweka Hazina na
4. Wajumbe wawili wa Kamati Tendaji.

Uchaguzi huo unatarajiwa kufanyika siku ya Alhamis tarehe 25 Februari, 2021. Hivyo, kwa wale wajumbe wote wenye nia ya kugombea nafasi hizo wanaombwa kuchukua fomu katika Ofisi ya Divisheni ya Ushauri wa Kisheria leo hii kuanzia saa 4:30 asubuhi, na fomu hizo zinatakiwa kurejeshwa sio zaidi ya saa 7:00 za mchana leo hii. Ahsanteni sana waheshimiwa.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Mhe. Spika, nimesimama hapa kwa Kanuni ya 63 ila nina hoja kwa Kanuni ya 42. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja ya dharura kuhusiana na kuzuiliwa kwa bodaboda na bajaji kuingia katika eneo la Mji Mkongwe wa Zanzibar kuanzia tarehe 01 Machi, 2021.

**Mhe. Spika:** Mheshimiwa unakusudia kuileta hiyo hoja kwamba tuijadili kwa muda wa saa maana yake kwa utaratibu itabidi tuijadili kwa saa nzima.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Mhe. Spika, hoja hii naomba isijadiliwe.

**Mhe. Spika:** Kwa hiyo, unaweza ukaiwasilisha halafu serikali itasikia itakuletea majibu, endelea nakuruhusu.

### HOJA YA MJUMBE

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Ahsante Mhe. Spika, hoja ya dharura kuhusiana na kuzuiliwa kwa bodaboda na bajaji kuingia katika eneo la Mji Mkongwe wa Zanzibar kuanzia tarehe 01

Machi, 2021 imefanywa chini ya Kanuni ya 27(1n), 27(3) na 42 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi za Mwaka 2020.

Mhe. Spika, maelezo ya hoja ni kwa kuwa vituo vya kushushia abiria vinavyotumiwa na gari za abiria maarufu kama (daladala) vipo mbali na eneo la bandarini, na kwa kuwa asilimia kubwa ya wananchi wanaosafiri kwa kutumia bandari hawana usafiri binafsi na hutegemea bodaboda au bajaji.

Kwa kuwa asilimia kubwa ya wananchi wetu vipato vyao ni vya chini hivyo hawana fedha za kukodia magari ama *taxi* na hutegemea usafiri wa vyombo hivyo ambavyo vinawapa urahisi, na kwa kuwa wananchi wengi hubeba wakati wa kusafiri. Hivyo basi, mimi Shaib Hassan Kaduara, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Chake Chake chini ya Kanuni ya 27(1n) na 27(3) na Kanuni ya 42 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2020 napendekeza mambo yafuatayo:

Serikali kuliangalia upya suala hilo kwa maslahi ya wananchi wetu, serikali kuweka utaratibu maalum wa usafiri utakaowawezesha wananchi kufika na kutoka bandarini kwa wakati bila ya usumbufu wowote, kuwe na utaratibu utakaowekwa na serikali ili kuwe na unafuu kwa wananchi wa kipato cha chini kunufaika na bandari.

Mhe. Spika, basi serikali ingefukia maeneo ya Bwawani ili daladala ziweze kuzunguka pale na kushusha watu na kuondoka ili wasipate usumbufu. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha hoja.

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Shaibu Hassan Kaduara, samahani serikali ilichukue ili ikalifanyie kazi na baadae tuletewe majibu kwa sababu ni la dharura nisingeweza kutoa muda hapa tulijadili kwa saa nzima, kwa sababu tuna shughuli nyengine ambazo ni za muhimu tunataka tuzifanye vile vile. Kwa hiyo, nafikiri serikali wamesikia na wamelichukua wahusika wapo humu ndani na majibu yanaweza kupatikana bila shaka yoyote. Ahsante.

## HOJA ZA SERIKALI

### Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali, 2021

*(Kusomwa mara ya kwanza)*

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na utukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema kutuwezesha kukutana hapa leo hii kwa dhamira ya kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kumpa pole Mhe. Rais wa Zanzibar kwa msiba wa Makamu wa Kwanza wa Rais (Maalim Seif Sharif Hamad) na kwa pamoja basi tunaungana kumuombea kwa Mwenyezi Mungu ampe makaazi mema na kuipa familia yake subra katika msiba huu mkubwa.

Mhe. Spika, aidha nakushukuru na kukupongeza wewe Mhe. Spika, kwa jitihada zako na namna unavyoliongoza Baraza hili tukufu kwa ustadi na upeo mkubwa. Ni imani yangu kwamba utaendelea kutuongoza kwa uadilifu na ustadi wa hali ya juu kwa lengo la kusimamia chombo hiki pamoja na ustawi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa pamoja na wajumbe wake wote kwa jinsi walivyoupokea mswada huu na kuweza kutoa michango yao mizuri na hatimae kuukubali.

Mhe. Spika, madhumuni ya kuletwa kwa mswada huu ni kufanya marekebisho katika baadhi ya vifungu vya sheria mbali mbali kwa ajili ya kuweka masharti bora zaidi na yenye kuleta ufanisi wa utekelezaji wa sheria hizo.

Mhe. Spika, sheria zilizofanyiwa marekebisho katika mswada huu ni Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam. 7 ya 2018 na Sheria ya Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Nam. 8 ya 2015.

Mhe. Spika, pamoja na maelezo haya mswada huu umegawanyika katika sehemu kuu tatu. Mhe. Spika, sehemu ya kwanza ya mswada inahusiana na masharti ya awali ambayo yanaelezea jina fupi na kuanza kutumika kwa sheria hii.

Mhe. Spika, sehemu ya pili ya mswada huu inaweka mapendekezo ya marekebisho yaliyopo chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam. 7 ya 2018 katika kifungu cha 151. Aidha, mapendekezo ya marekebisho chini ya kifungu hiki yana madhumuni ya kufuta na badala yake ukikiandika upya kifungu hiki kwa lengo la kuleta ufanisi katika utekelezaji wa sheria hiyo.

Mhe. Spika, kwa mnasaba huo serikali iliona ipo haja ya kukipitia upya kwa kifungu 151 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam. 7 ya 2018 na kufanya marekebisho ambayo yataondosha kabisa uwezekano wa kutoa dhamana kwa makosa yasiyokuwa na dhamana yaani *non bailable offences.*

Mhe. Spika, vile vile sehemu ya tatu ya mswada huu inapendekeza baadhi ya marekebisho katika sheria ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi Nam. 8 ya 2015 katika vifungu vya 2, 3, 9, 13, 14, 15, 19, 20, 25, 30, 38, 44, 46, 59 na 67.

Mapendekezo ya marekebisho ama kwa madhumuni ya kufuta kuweka badala yake na kuipa nambari mpya. Sehemu hii pia imependekeza masharti kwa ajili ya kuongeza vifungu vidogo vipya katika vifungu vya 30 na 44 pamoja na kuongeza vifungu vyengine vipya vya 44A, 44B na 44C.

Mhe. Spika, Marekebisho ya Sheria ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Nam.8 ya Mwaka 2015 yanatarajiwa kuvutia zaidi wawekezaji na kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya umma na utoaji wa huduma, kuhamisha vichocheo hatarishi kutoka upande wa serikali kwa kuzingatia uimarishaji wa urithi wa Zanzibar,

uhifadhi na ulinzi wa mazingira pamoja na kuongeza ushindani katika miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, vile vile marekebisho haya yanatokana na dhamira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Nane kutaka kukuza maeneo ya uwekezaji kwa kufanya kazi kwa pamoja baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa lengo la kukuza uchumi na hatimae kutoa huduma bora kwa jamii ikiwemo huduma za afya, elimu na miundombinu ya umma.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Mhe. Spika:** Ahsante. Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Mhe. Mwanasheria Mkuu kumradhi kwa sababu mswada huu umekuja kwa hati ya dharura. Kwa hivyo, ningekuomba uisome hiyo hati ili iweze kuingia kwenye *hansard*. Tafadhali Mhe. Mwanasheria Mkuu.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, Mswada huu kama ambavyo Mheshimiwa umesema umekuja kwa hati ya dharura kwa Tangazo Nam. 50 kupitia Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2020 chini ya Kanuni ya 81 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi na inasema kama ifuatavyo:

> "Kwa uwezo niliopewa chini ya Kanuni ya 81 Kanuni ya Baraza la Wawakilishi Toleo la 2020, Mimi Dokta Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi natamka kwamba, Mswada wa Serikali wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani yake ni wa dharura na wa haraka sana na kuwa hauwezekani kutimiza masharti ya Kanuni ya 88 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi."

Imetiwa saini na muhuri wa Mhe. Rais tarehe 18 Februari, 2021. Mhe. Spika, nakushukuru.*(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa usomaji wa hiyo hati ya dharura. Waheshimiwa hoja imetolewa na imeungwa mkono na upande wa serikali, sasa sitowahoji naomba tuingie kwenye mjadala, lakini kwanza nimkaribishe Mhe. Hassan Khamis Hafidh, Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Mhe. Spika, awali ya yote naanza kwa kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kutekeleza majukumu yetu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutubariki amani na upendo, busara na hekima, pamoja na neema zote ambazo ni muhimu sana kwetu.

Mhe. Spika, pili naomba kuchukua fursa hii kumpa pole Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kufiwa na Makamu wake wa Kwanza wa Rais Marehemu Seif Sharif Hamad. Lakini kadhalika naomba kutoa fursa hii kuwapa pole Wazanzibari wote na Watanzania kwa jumla kwa kufiwa na kiongozi wetu, mzee wetu Marehemu Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Spika, tatu, napenda kuchukua fursa hii pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika Mkutano huu wa Pili wa Baraza lako tukufu katika kuchangia na kuuboresha mswada huu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu akuzidishie hekima na busara katika kutekeleza majukumu yako ya kila siku.

Mhe. Spika, aidha, pongezi za dhati kabisa ziende kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar kwa mashirikiano makubwa kwa kamati wakati ilipokuwa ikijadili mswada huu, pamoja na juhudi zao za kuzifanyia marekebisho sheria zetu muhimu kwa ajili ya kuleta ufanisi.

Mhe. Spika, pia shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano yao makubwa waliyotoa kwangu na juhudi zao wakati wa kuujadili kwa kina mswada huu.

Mhe. Spika, naomba sasa uniruhusu niwataje Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu |
| 3. | Mhe. Machano Othman Said | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Haji Jecha Salum | Katibu |
| 9. | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu na |
| 1( | Ndg. Amina Abeid Hemed | Msaidizi wa Mjumbe |

Mhe. Spika, naomba sasa uniruhusu nieleze baadhi ya marekebisho na mapendekezo ambayo kamati yetu imeyafanyia, licha ya kuwa mswada huu hauna kasoro nyingi. Vile vile, naomba kuwaeleza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwa hotuba hii inatoa ufafanuzi tu na msisitizo wa baadhi ya vifungu ambavyo vimependekezwa kufanyiwa marekebisho. Hivyo, maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yanaonekana katika Marekebisho ya Kamati ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshapatiwa kwa ajili ya ufafanuzi na ufahamu zaidi.

Mhe. Spika, kamati inashauri katika kifungu cha *4* kufutwa maneno "makosa yasiyo na dhamana" yaliopo mwishoni mwa kifungu hicho na badala yake kuwekwa maneno "kosa lisilo na dhamana", ili kwenda sambamba na Sheria Mama.

Mhe. Spika, Kifungu cha 8 kinashauriwa kurekebishwa kwa kufutwa neno *"*nakuweka*"* liliopo baina ya nambari 67 na neno "badala yake" ili kuweka usahihi wa uandishi.

**HITIMISHO**

Mhe. Spika, nina imani kubwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu wanakubaliana na maoni ya kamati katika mswada huu ili lengo la serikali kuzifanyia marekebisho sheria hizi liweze kufikiwa.

Mhe. Spika, sambamba na hayo, kamati yangu inawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waujadili na kuuchangia ipasavyo mswada huu ili hatimae kuupitisha ili sheria hiyo ambayo itaziwezesha taasisi hizi kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kuwasilisha.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Hassan Khamis Hafidh, Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Waheshimiwa Wajumbe ninao wachangiaji na naomba niwataje. Kwanza kabisa atakuwa Mhe. Juma Makungu Juma ambaye atafuatiwa na Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na Mhe. Omar Said Shaaban ajiandae.

**Mhe. Juma Makungu Juma:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi nami kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbali Mbali. Lakini nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) kwa kuendelea kutujaalia uhai na uzima na kutuwezesha kufanya majukumu yetu kama ambavyo tumejipangia hapa Barazani.

Aidha, nimshukuru kwa dhati Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar kwa kuleta marekebisho haya kwa wakati muwafaka. Lakini pia niishukuru Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa namna ambavyo wameupitia mswada huu kwa kina na kwa ufupi wamerekebisha kila jambo ambalo tungepaswa kuliona au kulisema. Lakini kwa vile ni utaratibu basi naomba na mimi nichangie yale machache ambayo nimeyaona aidha kwa kukazia au mengine mapya kwa ajili ya kuweka mswada wetu kuwa bora zaidi.

Mhe. Spika, mimi nitaanza na kifungu cha 151 kwa sababu hiki ni kipengele kikubwa sana na ni muhimu sana na hasa ukizingatia kwamba jamii yetu imekumbwa na wimbi kubwa la udhalilishaji. Kipengele hiki kinalenga katika kuyapunguza makosa kama si kuyamaliza kabisa.

Mhe. Spika, kipengele hiki cha 151(1) kimeanza kusema “Pale mtu yeyote asiyekuwa mtu anayeshitakiwa kwa kuuwa kwa kukusudia uhaini, unyang’anyi wa kutumia silaha, kukutwa na silaha, kusafirisha dawa za kulevya, kosa linalohusu kiwango kikubwa cha dawa za kulevya, kubaka, kuingilia kinyume na maumbile, kunajisi mtoto wa kiume…”. Sasa mimi swali langu liko hapa. Kunajisi mtoto wa kiume inatofautiana vipi na hilo lilikuwa limetangulia mwanzo kuingilia kinyume na maumbile. Kama itakuwa iko tafauti kwa nini kwenye kipengele hiki sijaona kumnajisi mtoto wa kike, kama hii inafanana na hii hapa kwanini hii iwepo hapa. Sasa kama hii itakuwa haifanani basi nashauri na mtoto wa kike ionekane hapa imejitokeza na kama imejirejea hii basi hii hapa iondoke.

Ukiendelea mbele katika kifungu hicho utakuta “…kubaka kwa kikundi au kuingilia maharimu…”. Hapa pameandikwa ‘au’. Kamati wameona hili na wakasema iandikwe ‘,’ kitu ambacho na mimi naungana nacho kwamba hapa “au” iondoke iwekwe “ , ” ili iendelee kuingilia maharimu. “…kumnajisi mtu mwenye ugonjwa wa akili, utakatishaji wa fedha haramu, kukwepa kodi,” hapo pana ‘,’ “…matumizi mabaya ya mali…”.

Kamati wameshauri hapa kukwepa kodi au matumizi mabaya ya mali. Mimi naungana na kamati liwepo neno “au” kwa sababu hata ukiangalia hii ya Kiingereza imeandikwa hapa “*or*”. Sasa *or* kwa Kiswahili maana yake ni au, kwa hivyo hapa iandikwe hiyo au. Lakini pia ni kosa la mwisho katika kipengele hiki, kwa hivyo lazima ‘au’ ijitokeze na ionekane kwa usahihi.

Mhe. Spika, niende kwenye kifungu cha 44A, tayari hapa kamati wametusaidia wameliona hili kwenye kifungu (e) “mwekezaji mnafiki atalazimika kuharamia upembuzi yakinifu na na utafiti”. Kwa hivyo,  na moja bila shaka inaondoka lakini pia yale mengine ambayo wameshauri kamati kwenye kifungu hiki naunganayo. Lakini (e) ya pili bila shaka itabadilika na kuwa namba (f).

Mhe. Spika, katika kifungu 44B(1) hapa kamati wamerekebisha, “Endapo mwekezaji binafsi hajatimiza vigezo vilivyoainishwa chini ya kifungu cha…”. Hapa kamati wameiandika kitu ambacho kimekosekana hapa ni vyema kikawepo. “…ikiwa wazo la mradi ni sahihi mwekezaji binafsi anaweza kupewa fursa ya kufanya mapitio ya mradi uliowasilishwa ndani ya siku thelathini tokea tarehe maelekezo yalipotolewa”. Sasa hapa sijui tu Kiswahili Sanifu kikoje na kwa vile mimi natoka Matemwe mtazingatia, lakini nilidhani ingekaa ‘ya’ hapa baada ya ‘siku thelathini tokea tarehe ya maelekezo ilipotolewa’. Nadhani ingekuwa sahihi zaidi lakini Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora wa Kiswahili ataweka vizuri zaidi.

Mhe. Spika, baada ya hayo mimi niungane na kamati kwa sababu wamekwenda kwa kina kwa jili ya kuweka mswada wetu kuwa vizuri zaidi. Nashukuru ahsante sana kwa kunipa nafasi.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Juma Makungu Juma naomba sasa nimwite Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na Mhe. Omar Said Shaaban ajiandae.

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma:** Ahsante Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo hapa, lakini pia nikushukuru na wewe kunipa nafasi hii niweze kuchangia Mswada uliokuwepo mbele yetu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbali Mbali.

Pili, nichukue nafasi hii kumpongeza Mwanasheria Mkuu na timu yake ambao walikaa kwa pamoja wakaona ipo haja kutuletea marekebisho haya. Lakini pia nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutuletea hati ya dharura kuhusiana na suala zima la mswada huu.

Mhe. Spika, kabla sijaanza katika eneo hili na mimi kutoa mchango wangu kwanza niende kwenye Madhumuni na Sababu.

Mhe. Spika, "Madhumuni ya Mswada huu ni kufanya marekebisho kwa ajili ya kuweka masharti bora zaidi na yenye kuleta ufanisi wa utekelezaji wa sheria hizo. Sheria hizo zilizofanyiwa marekebisho katika mswada huu ni:-

1. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam. 7 ya Mwaka 2018". Ukiangalia ni juzi tu mswada huu tumeufanyia kazi.
2. "Sheria ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Nam. 8 ya Mwaka 2015". Niwapongeze sana inaonekana kuna vitu wameviona ndio maana wakaleta.

Mhe. Spika, lakini katika hii madhumuni na sababu kwa mfano katika hii Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai nilikuwa naomba sana Mhe. Spika kwa *AG* walikuwa watwambie ni sababu gani hata wakaona kwamba walete marekebisho haya, hasa ukizingatia ni juzi tu sheria hii tumeipitisha. Kwa hivyo, ilikuwa ioneshe katika hii madhumuni na sababu kwamba kuna sababu moja, mbili, tatu; kuna hiki na hiki tofauti na walivyotuwekea hapa. Kwa hivyo, nilikuwa naomba hilo ili wananchi waelewe labda kulikuwa kuna kitu gani au mkwamo gani katika kutekeleza sheria hii.

Mhe. Spika, cha pili nije moja kwa moja katika kifungu cha 151 "Uwezo wa jumla wa kutoa dhamana". Mheshimiwa katika kipindi kilichopita katika eneo hili Waheshimiwa Wajumbe wengi hapa tulikuwa wagumu sana kwa kifungu hiki kuwa kimetoa dhamana kama sikosei dhamana kwa Jaji Mkuu. Lakini tumeona kwamba hali ilikuwa mbaya na ndio maana wakaleta, kumbe watakubaliana na sisi watunga sheria wa humu Barazani kwamba lile ambalo tulilokuwa tukilisema na wao wakatupinga au wakaona kwa mujibu wa walivyoona inafaa, basi nadhani sisi tuwashukuru wajue kwamba na sisi ni sehemu ya watunga sheria. Kwa hivyo, yale ambayo tunayaona basi wakati mwengine wakubaliana na sisi.

Mhe. Spika, suala hili katika kifungu hiki kuna kifungu 151 lakini kuna (1), (2), (3), (4), (5) mpaka (6). Mwanasheria Mkuu anajua kifungu huwa kinasomwa chote kwa mujibu wa sheria ya tafsiri ya Sheria Nam. 7 ya Mwaka 84. Kwa maana hiyo, asije akanijibu hapa

akasema sisi tumekwenda katika kifungu cha 151 tu, lakini namkumbusha katika hiyo tafsiri ya sheria niliyoisema ya Nam. 7 inasema hivyo.

Sasa nije kwenye kifungu nambari 151(3), kimeandikwa "Kiwango cha dhamana kitapangwa kwa kuzingatia mazingira ya kesi husika na hakitokuwa kikubwa sana".

Mhe. Spika, hapa niwaombe sana Mwanasheria Mkuu na wataalamu wake waweke wazi katika hivyo viiwango vya dhamana. Kwa sababu wasiwasi wangu inawezekana kwa upande mwengine tukatoa mwanya kati ya polisi pamoja na mahakama. Kwa hivyo, nashauri sana katika kifungu hiki kiwekwe jadweli ambalo litaainisha viwango vya fedha kwa mujibu wa kesi husika, nimuombe hilo.

Mhe. Spika, tuje katika eneo hilo hilo kifungu cha 151 ambapo leo ndio kimeletwa, lakini sheria hii marekebisho haya yameleta sheria mbili tu, na katika marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam. 7 ya Mwaka 2018 ametuletea kifungu kimoja.

Mhe. Spika, nilitaka nimuulize *AG* sheria hii au kifungu hiki isijekuwa kimeletwa kwa sababu tu ya ile tuzime moto kwa sababu ya wananchi kuja juu kwenye mawio na kwenye mambo yote ambayo wananchi wetu wanazungumzia suala zima la dhamana, kutokupewa dhamana kwa hawa watu wanaowanajisi watoto au katika makosa hayo. Kwa hivyo, mimi wasiwasi wangu au nilikuwa namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu atwambie je, ni kwa kiasi gani Mwanasheria Mkuu na timu yake ya wataalamu wamepitia kwa kina kwa kila kifungu cha sheria kama kuna tatizo katika vifungu vyengine katika sheria hii.

Kwa nini nasema hivyo Mhe. Spika? Wasiwasi wangu kuwa tumekuja na kifungu kimoja cha dhamana lakini inawezekiana kuna matatizo ya udhalilishaji sio kwa dhamana tu, lakini pengine kuna mambo mengine mbali mbali ambayo yanaweza sheria hii ikawa ina mapungufu yake. Kwa hiyo, nilikuwa naona sheria hii au kwenye eneo la udhalilishaji kuna tatizo la mahakama zetu kutoa adhabu ndogo kwa wanaotiwa hatiani. Mfano, mtu anaweza kumlawiti mtoto au kumfanyia suala la kumuingilia kivyovyote vile aidha mwanawe au mtu mwengine. Lakini tunasikia kwenye mawio mtu anafungwa miaka saba, miaka mitao, mitatu au vyenginevyo.

Sasa hoja yangu Mheshimiwa *AG* pamoja na serikali basi tulikuwa tuitumie fursa hii ya leo hapa kuleta sheria za adhabu pamoja sheria ya mahakama za mahakimu ili kuwaongezea uwezo kutoa adhabu zaidi, na Mhe. Rais alisema kwamba hizi sheria ni za kwetu kwa hiyo chochote kile kinawezekana tukabadilisha. Sasa na mimi wasiwasi wangu kwamba pengine sisi tumeona kifungu cha dhamana lakini pia kuna tatizo katika sheria hii hii kwa upande mwengine. Sasa kama ni hivyo, basi nikuombe sana Mheshimiwa *AG* kama hamjkaa na wataalamu basi niwaombe mkae tena uzuri lakini ilikuwa toka mwanzo mngekaa vizuri nadhani tungepata fursa hii leo hapa ya kubadilisha hata katika maeneo mengine.

Mhe. Spika, kwa kweli suala hili linaumiza sana na nadhani tutakubaliana na wajumbe wenzangu wote kwamba moja katika kadhia kubwa ambayo kama imekuwa sugu ni hii moja ya udhalilishaji. Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu leo ametuletea hili, lakini

atwambie katika maeneo hayo niliyomwambia ni kwa kiasi gani wamekaa na wataalamu ili kuona hii sheria katika ile iliyosema kuhusiana na sheria ya adhabu.

Mheshimiwa lakini nije katika Sehemu ya Tatu kwenye Marekebisho ya Sheria Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Kifungu cha 11. Labda akija atwambie tu kwamba kifungu hichi kuna kitu gani mpaka wakaona kwamba badala ya Waziri wa Nchi, (OR) Fedha na Mipango waeke waziri husika labda kulikuwa na tatizo gani mpaka wakafikia katika hali hiyo.

Mhe. Spika, jengine katika Kifungu cha 9 katika Sehemu ya Tatu kimesema kwamba "Waziri anayehusika na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi anaweza kutengeneza kanuni zinazoelezea taratibu za uwekaji na ulipaji wa dhamana" iliyowekwa chini ya kifungu kidogo cha 7. Mheshimiwa mimi nilikuwa napendekeza kwamba, neno "anaweza" liondoke liwekwe "waziri anayehusika na mashirikiano ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi atengeneze kanuni zinazoelezea taratibu za uwekaji na ulipaji wa dhamana" iliyowekwa chini ya kifungu kidogo cha 7.

Mheshimiwa kwa nini nasema hivi, ukiangalia huko tunakotoka mara nyingi vifungu kama hivi sana Waheshimiwa Mawaziri wanakuwa hawatengenezi hizo kanuni kwa sababu wanatakiwa tu aweze. Kwa hiyo, Mheshimiwa naona ananiwashia taa, nilikuwa nataka nisome na hichi Kifungu cha 44(c) ambacho moja kwa moja kimeonesha kwamba "Timu ya majadiliano kwenye *marginal note* yake kutakuwa na Timu ya Majadiliano ya Serikali ambayo muundo wake, majukumu na uwezo kama utakavyoelezwa katika kanuni". Kwa hiyo, nasimamia hoja yangu hapa ili kifungu hichi kifanye kazi vizuri isiwekwe "anaweza" iwekwe tu "atengeneze" kwa sababu tayari imeonekana katika sheria hii lazima iwepo kanuni.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono kwa asilimia 99 mpaka Mheshimiwa *AG* atakapokuja kutupa maelezo ya kutosheleza na yenye kutuafiki katika mswada huu. Ahsante Mhe. Spika nashukuru.

**Mhe. Spika:** Ahsante, naomba sasa nimwite Mhe. Omar Said Shaaban na Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis ajiandae.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa asubuhi hii na mimi kuchangia Mswada huu wa Mabadiliko ya Sheria Mbali Mbali ambao umeletwa mbele yetu hapa na mwalimu wangu Dkt. Mwinyi Talib Haji. Lakini Mhe. Spika, kabla sijaendelea na mimi niungane na Waafrika wote duniani kwa kuipongeza timu ya Simba *Sports Club* kwa ushindi mzito, ambao kwa kweli unaipeleka nchi yetu Tanzania na tunaliona kombe la dunia la vilabu hilo hapo tukishiriki, na mimi nau-*dedicate* ushindi ule kwa Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sasa niende kwenye hoja, Mhe Spika, na nimpongeze tena Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kuleta mswada huu lakini na mimi pia niipongeze kamati kwa kazi yao ya kikanuni waliyoifanya ya kuona yale ambayo kamati imefanikiwa kuyaona kwenye mswada huu.

Mhe. Spika leo Baraza hili linalazimika kujadili mabadiliko haya ya sheria kutoka sheria ya mwaka 2018 kama alivyosema Mhe. Mwanaasha Khamis Juma kwamba ni muda mfupi tu sasa tunafanyia marekebisho Kifungu cha 151 cha Sheria Mwenendo wa Makosa ya Jinai, na hili halina wasiwasi ni kwa sababu tulipotunga, Baraza hili lilipofanya marekebisho ya sheria hii mwaka 2018. Kifungu hichi ni moja kati ya vifungu vilivyoleta mjadala na sisi wengine tulikuwa nje ya Baraza hili lakini tulikuwa tunafuatilia kilikuwa ni kifungu chenye ukakasi, tulikuwa tuna lugha zinatumika huko nje kwamba kutunga kifungu cha dhamana kinachompa mamlaka Jaji Mkuu peke yake, kutoa dhamana ilikuwa ni kufunga maduka lakini uzoefu umeonesha kwamba tumefunga maduka, tukafungua *super market.* Dhamana zikawa zinatoka nyingi kwa sababu kifungu kile kilikuwa sio *realistic* katika *practice* ya sheria.

Mhe. Spika, nataka kutoa indhari ya mapendekezo yaliyokuja safari hii. Kwanza kuongeza makosa yasiyokuwa na dhamana, indhari yangu Mhe. Spika iko kwenye katiba. Katiba yetu ya Zanzibar Ibara ya 13, Ibara ndogo ya 6 aya ya (a) inasema na naomba ninukuu.

"Kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria serikali itaweka taratibu zinazofaa na zitakazozingatia misingi kwamba wakati haki na wajibu wa mtu yeyote vinahitaji kufanyiwa uamuzi wa mahakama au chombo chenginecho kinachohusika basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa na pia haki ya kukata rufaa..."

Mhe. Spika, tunapotunga sheria kunyima dhamana kwa makosa haya ambayo tumeyaainisha. Maana yake kuna haki ya uhuru wa mtu au ya mtuhumiwa inafanyiwa maamuzi katika hatua za awali, haki ya kukaa ndani wakati shauri lake linaendelea. Mhe. Spika, mimi sina tatizo tuwe na utaratibu kwamba kuna makosa yasiwe na dhamana, lakini vipi tuna-*consider* matakwa ya katiba ya kutaka sasa huyu mtu asikilizwe kwamba *either* apewe dhamana kwa maana akakae ndani au asikae ndani, *enactment* hii Mhe. Spika kwa ilivyo, inavunja msingi huo wa katiba na itakuwa kosa kwa Baraza hili kutunga sheria ambayo inaenda kuvunja msingi wa katiba.

Tumepigia kelele huko wengine kabla hatujaingia humu kwamba *enactment* za namna hii ambazo zinakiuka katiba ni hatari kwa taifa letu, na nasema hivi Mheshimiwa kwa sababu *practice* imebadilika na uzoefu vile vile umebadilika. Tumeona pamoja kwamba jamii inapiga kelele kuhusu kuongezeka kwa makosa ya udhalilishaji, lakini tusisahau pia jamii inapiga kelele kuhusu watu kubambikiziwa kesi pasipokuwa na sababu za msingi. Tukiyaongeza makosa haya leo nikitaka mimi Mhe. Spika ukae ndani nitaripoti kwamba umemdhalilisha mwanangu yaani ni *blank check, State Attorney* anapofungua unapoandikiwa *charge sheet* ya namna hiyo maana yake huulizwi wewe kwamba ukae au usikae kwanza ni *blank check* kwamba lazima uende ndani kwanza.

Sasa hiyo ni hatari na bahati mbaya na nitaomba Mwanasheria Mkuu aje atujibu tunapoongeza makosa haya yasiyokuwa na dhamana na tunajua *practice* mahakama zetu zinachelewa sana katika usikilizaji wa mashauri. Kuna kesi zinakaa miaka mitano, sita, saba hazishi na hatimae watu wale wanakosa kutiwa hatiani, aje Mwanasheria Mkuu atueleze serikali sasa haioni haja ya kuwa na kifungu cha wale ambao wamewekwa ndani kwa kukosa dhamana, kwa sababu wamepewa makosa yasiyokuwa na dhamana, lakini mahakama haikuwatia hatiani wamepoteza

muda wa miaka miwili, mitatu, minne, saba gerezani. Vipi mpango wa fidia wa watu wa namna hiyo kwa sababu na wao ni jamii ambao wametumikia muda ndani.

Kwa hiyo, pamoja na kwamba kuongezeka kwa makosa haya tunahitaji kuwa na wawekwe ndani lakini tunahitaji pia kulinda haki za watuhumiwa. Mheshimiwa haki za watuhumiwa ni wajibu wa serikali kulipa sio mawakili wa utetezi peke yao. Serikali ina wajibu wa kulinda haki za watuhumiwa na hilo limeelezwa pia na katiba yetu hii hii ukisoma Ibara ya 14, ibara ndogo ya 2 inasisitiza hiyo kwamba "Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na kuishi kwa uhuru itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa au kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vyenginevyo isipokuwa tu katika hali ya kufuata utaratibu uliowekwa na sheria".

Sasa tunapo-*enactment* kwamba watu kuna makosa hayana dhamana. Je, anapokuwa mtu na kanuni ya kisheria iko wazi kabisa, kila mtu ni *innocent until proved guilt* sasa mtu anapokuwa mahakamani, na mahakama ikakosa kumtia hatiani na ameshatumikia ndani muda mrefu. Vipi mpango wa serikali kuwafidia wale ambao mahakama haikuwatia hatiani katika ngazi zote zile mpaka wamefika Mahakama ya Rufaa hakutiwa hatiani kumfidia huyu mtu ili muda aliopoteza na hili Mhe. Spika, nalisema Mhe. Mwanasheria Mkuu atakubaliana na mimi *position* ime-*change* safari hii tuna kesi za Mahakama Kuu zinazosema kwamba, ni wajibu wa *State Attorney* kuthibitisha kwamba mbele ya mahakama kwanini mtu huyo anyimwe dhamana. Yaani *the first place* sio mtu kwenda kuomba dhamana kusema kwamba anahitaji kuwa nje.

Mhe. Spika, kwa hivyo naomba tuwe na indhari kubwa sana, na nasema hili kwa sababu Mhe. Spika sisi wengine kwa bahati nzuri niseme tume *defence council* kwa muda huo kipindi chote cha miaka kumi. Wawakilishi, wananchi ndio wateja wetu hawa hawa, pamoja na kwamba tuna tatizo hili na mimi nakubaliana kabisa *strict measures* zichukuliwe na mwisho nitamalizia kwa kusema chengine, lakini tunahitaji kulinda haki ya kila mmoja. Haki ya *victims* na haki za watuhumiwa hatuwezi ku-*ignore* haki za watuhumiwa tuka-*concentrate* kwenye haki za *victim* peke yao ni wajibu wa serikali kikatiba kulinda haki za watuhumiwa.

Mhe. Spika, nataka kumalizia kwa kusema kwamba Mwanasheria Mkuu pia aje atueleze *focus* ya serikali ni ipi katika ku-*prevent crimes,* kwa sababu makosa ya udhalilishaji sio vita vya kisheria ni vita vya kimaadili. Jamii imekosa maadili hapa hata tukija tukitunga sheria kwamba wadhalilishaji wanyongwe wataendela kuwepo, kama ambavyo makosa mengine yanasema kwamba adhabu yake ni kunyongwa. Kwa mfano *murder* adhabu yake ni kunyongwa lakini wauwaji kesi za *murder* zinaendelea kuwepo watu wanaendelea kuuwa wenzao. Kwa hiyo, ninachosema Mhe. Mwanasheria Mkuu aje atueleze mkakati wa serikali ni upi kuhakikisha kwamba wana-*prevent crimes* badala ya kuongeza adhabu za kisheria na *strategies* za kisheria kudhibiti haya makosa *moral strategies* za kuzuia makosa ni zipi.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja ya kwamba kuna haja ya kuongeza mkakati zaidi lakini pia na-*reserve* hoja zangu kwamba Mwanasheria Mkuu aje atupe ufafanuzi mkakati wa serikali katika kudhibiti makosa haya yasitokee na ni vipi wamejipanga kulinda haki za watuhumiwa kama ambavyo katiba inataka. Ahsante sana Mheshimiwa. (*Makofi*)

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Omar Said Shaaban kwa mchango wako naomba sasa nimwite Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis na Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum ajiandae.

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis:** Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia au kutoa mapendekezo yangu juu ya Marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai namba 7 ya mwaka 2018.

Mhe. Spika, moja kwa moja kwa kuokoa muda mimi niende katika Kifungu cha 151, kifungu kama kilivyoelezwa hapo:-

"Pale mtu yeyote asiyekuwa mtu anayeshtakiwa kwa kuua kwa kukusudia, uhaini, unyang'anyi wa kutumia silaha, kukutwa na silaha, kusafirisha dawa za kulevya, kosa linalohusu kiwango kikubwa cha dawa za kulevya, kubaka kuingilia kinyume na maumbile, kunajisi mtoto wa kiume, kubaka kwa kikundi au kuingilia maharimu, kumnajisi mtu mwenye ugonjwa wa akili".

Mheshimiwa hoja yangu ianzie hapa, kutokana na maelezo ya kifungu hichi hapa amezungumza mwenye ugonjwa wa akili, lakini kama ziku zote ninavyosema Mhe. Spika kwamba kuna tofauti baina ya mgonjwa wa akili na mlemavu wa akili. Mgonjwa wa akili anapata tu yale maradhi kwa muda baadae anakuwa katika hali ya kawaida, lakini mlemavu wa akili maishani mwake inakuwa ni hali ile ile. Kutokana na changamoto hii ya kubakwa wengi wanaokutana na changamoto hii ni wenye ulemavu wa akili, kwa sababu hawezi kujieleza wala hawajui kitu.

Kwa hivyo, mimi mawazo yangu au mchango wangu naomba hapa tufanye marekebisho aidha, badala ya kusema "mwenye ugonjwa wa akili" tuseme "mwenye ulemavu wa akili" iendane na huu mswada wa Kiingereza kwa sababu umesema "*person with mental disability".* Kwa hiyo, au badala ya maneno haya tuongeze "mtu mwengine mwenye ulemavu wa aina yoyote" kama tunataka hii ibakie kama ilivyo nishauri tuongeze neno tuongeze neno "mtu mwengine mwenye ulemavu wa aina yoyote". Kwa sababu hao wanaofanya vitendo hivi mara niyngi hukimbilia wenye ulemavu kwa sababu kutokana na hali zao, wanachukulia kwamba kutokana na maumbile yao pengine wengine ndio kama hivyo wanashindwa kujieleza, lakini kutokana na hali zao wengine wanakuwa wanasamehe au changamoto mbali mbali zinakuwa zinawakumba. Kwa hivyo, Mhe. Spika ningeomba hapa tukafanya marekebisho hayo.

Lakini cha pili, inasema "pamoja na kukwepa kodi" yaani mtu ambaye anakwepa kodi hatokuwa na dhamana kwa nilivyo fahamu hapa, lakini ningeomba ikaelezwa au ikafafanuliwa ni kiwango gani cha kodi ambacho kimekwepwa. Kwa sababu isijekuwa mama ntilie hajalipa kodi ya 2000/- akakumbwa na sheria na kifungu hichi kikamhukumu. Kwa hiyo, hapa ningeomba tukafanyiwa ufafanuzi tukapewa ufafanuzi na ikafafanuliwa ni kiwango gani cha kodi ambacho kimekusudiwa hapa. Lakini pia matumizi mabaya ya mali, pia nayo Mhe. Mwanasheria Mkuu akija atufafanulie matumizi mabaya ya mali zipi ambazo zimekusudiwa hapa.

Mhe. Spika nikija Kifungu cha 151(2) kama kinavyosomeka hapo nacho pia ningeomba tuongeze maneno mwanzo na mwisho wa kifungu hiki. Kwa sababu msingi wa kifungu hiki kinatokana na kifungu cha 151. Kwa hivyo, kifungu hicho hapa kimeanza na mkuu huyo wa kituo, kama hakuna mashiko fulani. Lakini ningependekeza ili kukihusisha na kifungu cha

151(1) tuongeze neno "kwa mujibu wa kifungu kidogo cha kwanza, mkuu huyo wa kituo" iendelee kama ilivyo.

Mwisho tumalizie "wadhamini kwa ajili ya kuhudhuria kwake kama itakavyoelezwa baadae". Ningependekeza tusiishie "baadae" tuongeze neno "kwa kutegemea uzito wa kesi". Kwa sababu kuna makosa mengine yanakuwa ni makubwa. Kwa hiyo, tukisema kwamba dhamana yake anaweza akaachiwa yeye mwenyewe kidogo itakuwa pengine mtu anaweza akatoroka au ikatolewa uzito mkubwa wa kesi lakini dhamana ikawa ni ndogo.

Nikija kifungu kidogo cha tatu, kiwango cha dhamana kitapangwa kwa kuzingatia mazingira ya kesi husika na hakitokuwa kikubwa saa. Mhe. Spika, mimi ningeomba hii "hakitokuwa kikubwa sana" tuiondoe kwa sababu kuna kesi nyengine lazima kiwango chake cha dhamana kiwe kikubwa ili kumzuia mtuhumiwa asije akatoroka.

Mhe. Spika, nikija kifungu kidogo cha nne, Mahkama kuu inaweza katika kesi ya makosa yenye dhamana kuelekeza kwamba mtu yoyote apewe dhamana au masharti ya dhamana yaliyowekwa na Mahkama ya Chini au polisi yapunguzwe. Mhe. Spika, ningeomba au ningependekeza tukaongeza neno "au yaongezwe", ili kama mahkama imetoa dhamana ndogo kulingana na kosa lilofanyika, hapa Mahkama Kuu iweze kuongeza au kutoa maelekezo kwa Mahkama ya Chini ili kiwango kile kilichotolewa ni kidogo kwa mujibu wa uzito wa kesi yenyewe.

Mhe. Spika, tukisema ipunguzwe sasa sifikirii kama kutakuwa na kesi kubwa halafu kiwango cha dhamana kikawa kimetolewa kidogo kikaweza kuongezwa. Kwa hiyo, hapa ningependekeza tu tukaongeza neno, baada ya neno "yapungunguzwe" tuongeze neno "au yaongezwe". Mhe. Spika, nakushukuru Ahsante.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Nakushukuru sana Mhe. Spika, na nampongeza Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Mwenyekiti wa Kamati hii kwa maoni yao. Mwanasheria Mkuu kwa kuleta hii *miscellaneous amendments* lakini Mwenyekiti wa Kamati kwa maoni ambayo ameyatoa. Mimi nina maeneo machache tu ambayo natataka ufafanuzi na pengine kama sijapata ufafanuzi unaojitosheleza nadhani tutaweka vizuri wakati wa vifungu.

Mhe. Spika, kwenye Sehemu ya Pili ya Marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai namba 7 ya mwaka 2018. Kwanza naipongeza sana sana serikali. Hii inaonyesha jinsi gani serikali yetu ilivyokuwa sikivu kwa sababu sisi tumepiga sana kelele kuhusiana na haya makosa ya udhaliliishaji na jinsi gani mazingira yanafanya washtumiwa au wahutumiwa, sijui wanaitwaje, wale wanaokamatwa, washtumiwa wanavyokuwa wanakwepa sana mkondo wa sheria kwa sababu ya *weaknesses* za kwenye sheria zenyewe.

Kwa hiyo, mimi naipongeza serikali kuja na marekebisho haya. Lakini nna *concern* kwenye kifungu hichi cha 151(1). Kifungu hichi marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai naona kime-*accommodate* mambo mengi kwa wakati mmoja *in such a way* mpaka kunawa na *confusion* ya *which is which*. Marekebisho yetu hasa tulikuwa tunataka yafanyike kwenye masuala ya udhalilishaji na ndipo ambapo tulikuwa tunataka pini ibane zaidi. Najua kwamba

hicho kifungu kwenye sheria mama ina-*contain* vifungu hivi ambavyo vimewekwa labda pengine vimeongezwa.

Mhe. Spika, masuala ya kukwepa kodi. Mimi nashauri mwanasheria Mkuu tungekwenda katika *definition* zaidi. Kukwepa kodi tu ukaiweka pale halafu ikawa *just* kukwepa kodi. Juzi hapa tulizungumzia masuala ya *ZAECA*. Umekwepa kodi au hujalipa labada kwa sababu ya *inconvenience* nyengine lakini unakuwa *subject to scrutiny* kupelekwa katika vyombo vyengine.

Kwa hivyo, hili linaweza likatumika. Hatuhamasishi watu kukwepa kodi *in fact* tunataka watu walipe kodi. Lakini kuwe kuna mazingira zaidi ya watu kulipa kodi yaani *easiness* ya kulipa kodi isiwe *hard in such a way* mtu anakuwa *subjected to* kutokwenda kulipa kodi. Kwa hivyo, mimi naomba kwamba vile vifungu ambavyo vinakuwa havi-*relate to* kifungu chenyewe kwa ujumla wake vingeekewa vifungu vyake ili kuwe kuna maelezo ya ziada ni jinsi gani mtu kama huyo kwa mfano hapa hatopewa dhamana ikiwa ameshutumiwa au ametuhumia kwa kukwepa kodi. Mazingira ya kukwepa kodi yakoje. Kwa hivyo, hapa Mhe. Mwanasheria Mkuu nadhani ingekuwa vizuri zaidi tungeweka vizuri. Vile vile, matumizi mabaya ya mali. Kungekuwa kuna maelezo matumizi mabaya ya mali mpaka mtu anafika kwamba hapewi dhamana ni yepi, inahitaji maelezo zaidi kuliko hapa tulivyokuwa tumeweka.

Mhe. Spika, kwenye kifungu hicho hicho namba tatu. kiwango cha dhamana kitapangwa kwa kuzingatia mazingira ya kesi husika na hakitokuwa kikubwa sana. Sasa nilikuwa najiuliza hii hakitokuwa kikubwa sana *definition* yake ikoje. *Factors* zake za kusema kwamba hii sio kikubwa sana, nini tuna-*determine how* kwamba hii dhamana au kiwango cha dhamana sio kikubwa sana. Laki tano kwa watu wengine inakuwa ni kubwa sana na kwa watu wengine si kubwa sana. lakini mbili inakuwa kidogo kwa watu wengine lakini wengine hawawezi ku-*afford*.

Mhe. Spika, sasa tukisema tu hii inakuwa *so subjective* kwamba kiwango cha dhamana kitapangwa kwa kuzingira ya kesi husika na hakitokuwa kikubwa sana naona kama inaleta ukakasi hivi, hakitokuwa kikubwa sana ni kama neno ambalo limewekwa. Hii inapelekea mahakimu wanapohukumu zile kesi wanakuwa *subjective*.

Mhe. Spika, juzi labda kama wiki mbili au wiki tatu zilizopita tumesikia hakimu mmoja amehukumu kesi, mtoto wa miaka ishirini nadhani ameshtumiwa kwa kubaka lakini amemuhukumu kwenda miaka 70 jela. Pengine inawezekana ikawa ni furaha *he is 20 years old* halafu amefungwa miaka 70. Kwa hivyo, hata akitoka hapa ni 90. *I don't know* kama kuna mtu anaweza akafika miaka 90 hapa.

Mhe. Spika, hii ni kwa sababu tunaweka sheria halafu *subject to* yule hakimu anavyoona. Lakini leo asubuhi nimesikia mwengine toka kuanzishwa Mahkama ya Kupinga vitendo vya udhalilishaji, amehukumu hiyo kesi na kijana nadhani ana miaka ishirini amefungwa miaka 40. 10 amefanya hivi sijui ametorosha na 30. Kwa hivyo, miaka 40. Sasa tuona kwamba ni vitu ambavyo kwa sababu tu ya hizi sheria tunafanya hukumu tunazozitoa ziwe *subjective* na ndio matatizo kama hivi tunavyoweka. Kiwango hiki hakitokuwa kikubwa sana lakini katika mazingira yepi unahesabu hichi kiwango sio kikubwa sana.

Mhe. Spika, maelezo mengine yapo katika Sheria hii ya PPP. Sheria ni sheria nzuri na tunajua kwamba sasa hivi mazingita *financing* yanabadilika na Masuala ya PPP yanatupa mwanga mpya kwa kuweza ku-*finance development programu* zetu ambazo zinahitaji fedha nyingi na kwa wakati huu serikali haitokuwa busara kuwekeza katika sera zile lakini inawezekana kuna wawekezaji binafsi ambao wako tayari katika kuwekeza katika miradi ya maendeleo.

Mhe. Spika, maelezo yangu yanakuja kwenye hichi kifungu cha 15 ambacho kinarekebisha kifungu cha Sheria mama kifungu cha 44. Kama kuna *confusion* lakini inawezekana Mhe. Mwanasheria Mkuu akija ataeleza vizuri zaidi. Mwekezaji binafsi ataalikwa kushiriki utaratibu wowote wa ushindani inakuwa ngumu sana kwenye Kiswahili lakini kifungu hichi cha 44(5) anasema mwekezaji binafsi anaweza kubarikiwa mkataba unaohusika na mradi aliouwasisi kwa taratibu wa ushindani wa zabuni chini ya sheria hii.

Mhe. Spika, anaweza mara nyengine miradi mikubwa mikubwa inaweza ikawa na washindani wawili watatu. Sasa hapa tunaweza tukamuondosha yupi, wa kwanza, wa pili, wa tatu, mradi anakuja lakini tunaweza tukamuondosha yupi kwa *factor* zipi. Hii Sheria ya PPP imeeleza hizo *factors* lakini bado kutakuwa kuna ugumu kwa sababu ukiweka hii PPP kwamba mtu anaekuja, yeye anavyoona ndio kinavyotekelezwa. Sisi kama serikali tunam-*scrutinize* vipi yule mtu kuona kwamba huyu anafaa na huyu hafai kwenye hivyo vigezo. Naomba viwekwe wazi ili tupate kufamu vigezo ambavyo vitatumika katika kum-*scrutinize* mtu.

Mhe. Spika, jambo jengine, sheria hiyo hiyo, tunarekebisha kifingu 44(c) katika haya marekebisho ya sheria, kifungu cha mwisho kabisa. 44(c) kinasema kwamba kutakuwa na timu ya majadiliano ya serikali ambayo muundo wake, majukumu na uwezo kama utakavyoelewa katika kanuni. Kanuni ni kitu kizuri.

Mhe. Spika, anaetayarisha kanuni ni Waziri. *He is a human being* ni binaadamu na kanuni zitapitia hizo lakini mwenye dhamana ya kanuni ni waziri. Hivi tutajuwaje yeye waziri anatekeleza majukukmu yake kwa kadri ya uwezo wake *in good faith* tutajuwaje. Sasa *for the sake* ya sheria hii, *for the sake* ya Miradi ya PPP ambayo ni miradi mikubwa ambayo *stake* ya serikali imo humo, tunataka hiyo *government negotiation team* iundwe katika sheria na tusimpe waziri aende akaunde katika kanuni.

Mhe. Spika, hii maana yake yule atakaeteuliwa katika hii *GNT* atakuwa ni *mas-ul* kwa nchi nzima yote na sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tutakuwa tumembariki tunampa hiyo dhamana. Hichi kifungu tutakuja kama hatujapata maelezo ya kujitosheleza hatuwezi kumpa dhamana kama hii ya serikali dhamana kubwa miradi huenda ikawa inachukua fedha nyingi, huenda ikawa tunataka kutoa tija kubwa kwa faida, huenda ikawa tunatoa dhamana kubwa kwa nchi tukamuwachia waziri yeye ndie akaunda *government negotiation team*.

Mifano tunaiona. Tunaona jinsi gani hata bodi tu za wakurugenzi, mtu anafikiria, bodi ya wakurugenzi anaweza akamuweka baba yake, bodi ya wakurugenzi atamuweka dada yake, bodi ya wakurugenzi anamuweka rafiki yake au shoga yake. *Simply* kwa sababu waziri tumempa dhamana aende akatengeneze kanuni na hatumuhoji kutokana ile kanuni.

Mhe. Spika, naomba wajumbe tutakisimamia hichi kipengele. Kifungu hichi *government negotiation team* iundwe kwa sheria na sio kanuni. Hili nataka kuweka wazi kwamba *GNT* kwa maana ya *Government Negotiation Team* itatumika tu kwa Miradi ya *PPP Government Negotiation Team* inatumika vile vile hata katika miradi ambayo ufadhili wake unakwenda katika *approaches* nyengine. Tuna *commercial loans* nyingi sasa hivi tunachukuwa, kuna taratibu nyengine za ufadhili wa miradi katika *aspect* mbali mbali.

Kwa hiyo tunataka *Government Negotiation Team* hii iwe inatumika vile vile kwenda kuangalia miradi mengine au kuangalia *mobilization of resources* katika miradi mengine, katika *approaches* nyengine *rather than PPP*. Tunaomba serikali ichukue haya mawazo. Iunde *GNT*, nia ni nzuri lakini iunde *GNT* kwa kupitia kwenye sheria yetu, tumjue nani atakuwemo katika *GNT*, wananchi tutamtizama, wawakilishi tutakuwa tunamtizama, mwenendo tutakuwa tunaujuwa na anaweza kuwa *subjected to scrutiny* tukiona mambo hayaendi vizuri.

Mhe. Spika, mimi yangu yalikuwa hayo, nakushkuru sana kwa nafasi na naunga mkono hoja kwa kiasi mpaka hapo ambapo nitapata maelezo mazuri zaidi. Ahsante.

**Mhe.Spika:** Ahsante sana Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum. Waheshimiwa Wajumbe huyo alikuwa ndie mchangiaji wetu wa mwisho naomba sasa nimwite mtoa hoja ili aweze kuhitimisha hii hoja.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, napenda kwanza kuchukua nafasi hii kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe ambao wamepata bahati ya kuchangia hoja hii ambayo imewasilishwa mbele ya Baraza lako tukufu na kwa hakika idadi yao wako kama sita, napenda kuwatambua kwanza kwa majina yao.

1) Mhe. Juma Makungu Juma
2) Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
3) Mhe. Omar Said Shaaban
4) Mhe. Mwanatatu Mbarak Khamis
5) Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum ambae ndie amemalizia.

Mhe. Spika, kwa hakika michango yao tumeisikia na kwa ujumla wake kama ambavyo nitajaribu kuyajibu, yale ambayo nimehisi kuna haja kuyajibu kwa uzito wake.

Mhe. Spika, Mhe. Juma Makungu Juma yeye baada ya pongezi alizungumzi kifungu cha 151(1) vipi kumnajisi mtoto inavyotofautiana na ile nyengine ya kumuingia kimaumbile. Ukiangalia sayansi ambayo imewekwa katika makosa hayo, tunajifunza kwamba jambo moja kubwa ambalo lipo. Makosa haya yalikuwa hayapo kabla ya 2018. Mabadiliko ya sheria ya 2018 ndio ambayo yameweza kuyaingiza hayo.

Mhe. Spika, kumnajisi mtoto wa kiume inatofautiana kabisa na kumuingilia mtu kinyume na maumbile. Kinyume na maumbile ina maana inaingiza zaidi ya mtoto wa kiume. Kwa hiyo, ina maana tunapokwenda kuyaangalia makosa haya yamewekwa pale kwa indhari maalum ya kuhakikihsha kwamba yana-*capture* yale mazingira yote ya dhana ya udhalilishaji.

Mhe. Spika, kwa ujumla wake makosa ambayo yalikuwa yapo pale yaliyoongezwa yalikuwa yana tija kwa kuona kwamba kwa wakati ambao tunakwenda nao ni vyema yakaongezwa na hasa katika nadharia nzima ya udhalilishaji lakini wakati huo huo kuhakikisha kwamba tunaondoa mianya ile ya uvujaji wa mali lakini poa ubadhirifu mali za umma. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ambacho nnaweza kusema ni kwamba hivi ni vitu viwili tofauti.

Mhe. Spika, nadhani mapendekezo yake mengine ni 44(a) maneno "ya na" kama ambavyo kamati imependekeza, kwa hakika hata sisi tumeweza kupokea na nimeyakubali yote. Lakini 44(b) neno ambalo limetokeza hapo ni kweli kabisa nayo tumeyaondoa kwa sababu nayo ni mapendekezo ya kamati na nina hakika kwamba tumeyakubali.

Mhe. Spika, upande wa Mhe. Mwanaasha Khamis Juma alikuwa anajaribu kusema madhumini na sababu hayakuonekana wazi katika mswada huu. Nadhani kilichokuwa kinakusudiwa katika mswada huu ni kwamba kuletwa kwa sheria inayohusiana na mwenendo wa makosa ya jinai. Kulikuwa na nadharia nzima ya kuhakikisha kwamba tunakwenda kupiga vita yale mazingira yote ambayo yanapelekea vitendo vya udhalilishaji.

Kwa hiyo, kuongezeka kwa makosa haya labda kumuingilia mtu ambae ni mgonjwa wa akili ina maana mwanzo halikuwepo na ukiangalia adhabu yake ni kifungo cha maisha. Lakini bado hakikuwa katika makosa ambayo hayana dhamana. Kwa hiyo, kuletwa huku pamoja na makosa haya ambayo yanaingiliana kwenye uhujumu uchumi katika *category* ambayo ni muhimu sana tumeona kwamba kwa sasa nchi yetu iko katika wakati huu kupambana na mambo haya na kwa uzito wake ndio maana tukaweza kuyaingiza. Kwa hiyo, sababu ambazo zipo ni kutokana na wakati na hasa kutokana na kongezeka makosa haya na kwa pamoja kuweza kuungana kwa pamoja kuweza kuyaondoa.

Mhe. Spika, pia aliulizia sababu za Sheria Nam. 7 ya 2018, imeletwa juzi tu lakini imeletwa tena kwa mabadiliko. Kama ambavyo nimesema mwanzo tunalo tatizo na sheria inakwenda kubadilika tulingana na wakati. Wakati tuliokuwa tunaitunga sheria hii 2018 pengine hatukuona umuhimu wa kuongeza makosa haya. Kama ambavyo nimesema awali, kuna makosa hayakuwepo kabla ya 2018 hapa. Kwa hiyo, kifungu hichi kimekuja kwa nadharia ya kusema pamoja kusema pamoja na kwamba mtu ana dhamana lakini kwa makosa haya yaliyotajwa mtu hatakuwa na dhamana ina maana kutakuwa na *purposive meaning* ya kuweka hivi vitu. Kwa upana wake dhamana ipo lakini kwa makosa haya na kwa uzito wake ndio maana yamewekwa kwamba hayana dhamana.

Lakini vile vile anahisi kwamba kama vile kimekuja zimamoto kifungu cha 151(1) si zimamoto ni *affirmative action* ya kuona kwamba tunaenda kutengeneza pale ambapo tumejua na Mhe. Spika, hii tunajua kama nilivyosema mwanzo sheria haiwezi kuwa *statistic* haiwezi kuganda tu pale pale ambapo ipo inaenda kulingana na mahitaji ya jamii husika na tumeona basi sasa na huu sio mwisho wa kifungu hichi kuongezwa itaendelea kuengezwa kwa makosa ambayo yataonekana kwamba ipo haja kwa wakati husika, kuweza kuingizwa ili yasiwe na dhamana.

Lakini pia Mhe. Mwanaasha Khamis Juma aliulizia juu ya mpango mkakati katika *issue* za udhalilishaji. Nadhani kupitia mabadiliko ya sheria hii tumeanza kuelekea kule ambako kupambana na nadharia nzima ya udhalilishaji.

Mhe. Spika, Wajumbe wengi ambao wamechangia wametuonesha na kwa hakika sote tunakubaliana kwamba kutungwa kwa sheria sio *conclusive remarks* kwamba tumeondokana na tatizo la udhalilishaji. Lakini kwa hakika ni hatua ya kuendea yale ambayo tunayataka na hasa tukitilia maanani Mhe. Spika, Mhe. Rais wetu amesema kabisa na namna ambavyo tunavyokwenda uanzishwaji wa Mahakama zinazohusiana na kushughulikia mambo ya udhalilishaji. Lakini Mahakama ili iende vizuri bila shaka tuwe pia na sheria nzuri imezungumzwa juu ya muitikio wa jamii ni hakika ni wajibu wetu sisi pamoja na watu wengine kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira sawa jamii nayo inaelimishwa. Kwa sababu wakati mwengine tunafahamu kunawezekana kubambikiana kesi. Lakini jamii itapofika pahali ikaelewa kwamba vita hivi ni vyetu sote na sisi kwa upande wetu wa serikali tumeanza na kwa hakika tutaendelea kuhakikisha kwamba vita hivi tunashinda sote kwa pamoja.

Lakini pia ametwambia katika marekebisho ya 11 kufuta Waziri wa Fedha na kumuweka Waziri anaehusiana na mambo ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma. Nadhani Mheshimiwa hii inatokana na mabadiliko ya muundo wa Serikali ya awamu ya nane. Ambapo mwanzo hii *department* inayohusiana na mambo ya Sekta Binafsi Sekta ya Umma ilikuwa chini ya Wizara ya Fedha kwa sasa hivi kwa vile ina-*move* inaenda kwa Mhe. Waziri wa Kazi na Uwekezaji ni dhahiri kwamba nalo pia linatakikana li-*move* liende kama ambavyo utaratibu wa serikali ambavyo unatakiwa uende.

Mhe. Spika, pia najielekeza kumjibu Mhe. Omar Said Shabaan ni ile ambayo amesema kwanza Mhe. Mwanaasha Khamis Juma kwamba muda mdogo ambao sheria inabadilika ni 2018 tu ni kweli. Lakini majibu yangu ni yale yale ambayo muda ndio ambao umetupeleke, yanayotokea ndio ambayo yametupelekea mahitaji tuliyonayo ndio ambayo imetupelekea tuwe na mabadiliko hayo ambayo tumekuwa nayo. Pongezi ambazo nimesema nadharia nzima ya kifungu kilichokuwa cha mwanzo katika Sheria mama ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai namba 154 kufutwa tumekileta kwa sababu tumefuta na kufunga ile milango yote ambayo makosa ya udhalilishaji yanaweza kuwa na dhamana. Lakini pia ameonesha indhari yake ya kwamba tunaongeza makosa mengi ambayo yatakuwa hayana dhamana, nadhani tukichukua na tukiyahesabu haya tunapochukua makosa yote ya jinai halafu ukatoa makosa haya ambayo yamewekwa hapa, ni dhahiri makosa ni machache sana na bila shaka kuna sababu yake maalum kwa nini yakawekwa hivi kulingana na mustakbali ambao tunaenda nayo.

Lakini pia alizungumzia kwamba namna ambavyo tunavyoyaoengeza tukumbuke mapendekezo ya vifungu mbali mbali vya katiba katika kuzingatia uhuru wa mtu. Ni vyema pia tukatambua katiba inajielekeza kweli kutoa uhuru wa mtu lakini bila shaka vile vile hicho kifungu cha 13 kinasema (a) kinasema: "Kulingana na sheria ambazo zitakazokuwepo".

Kwa hiyo, tunazotunga hizi Mheshimiwa ni sheria ambazo tunahakikisha kwamba tunaenda kutatua matatizo ambayo tunayo. Haiwezi tu kuwa kifungu cha sheria iko wazi kwamba kila

mmoja uhuru wake tu unalindwa watu wakafanya ambavyo wanavyotaka, hapana hii ni jamii na ni *nature* ya mwanaadamu anapenda kufanya yale ambayo mara nyingi anakatazwa.

Kwa hiyo, kama tutakuwa hatuna sheria mama ambazo ni msingi mkubwa sana wa kuzuia matatizo haya ni dhahiri kwamba *nature* ya mwanaadamu iko katika kufanya makosa ya sio kufanya yale ambayo ni ya kawaida.

Kutokana na hali hiyo, nimtoe tu wasi wasi ndugu yangu Mhe. Omar Seif Shaaban kwamba umakini kweli unahitajika. Lakini kwa umakini huu ndio maana hata uanzishwaji wa mahakama hizi zinazoelekea kusikiliza kesi za udhalilishaji tutakuwa makini sana kuhakikisha kwamba sheria zinaakisi mwenendo mzima wa makosa haya kama ambavyo muelekeo wa serikali yetu ya awamu ya nane inakusudia kwenda.

Lakini pia aliulizia Mhe. Omar Seif Shaaban kuhusiana na *focus* ya serikali kwamba tusijielekeze katika kubadilisha sheria. Ni kweli hili tumelichukuwa na kwa pamoja sisi serikali tu lakini sote kwa pamoja Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi kwa ujumla tupambane katika *moral aspect* maadili ya jamii yetu na kuhakikisha kwamba hatuwekewi vikwazo wale ambao wanatakiwa waendee mbele ya haki.

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis nae vile vile amejaribu kutoa mapendekezo yake kwa namna ambavyo alisema kwamba basi tuweke mtu mwenye ugonjwa wa akili au mwenye ulemavu wa akili. Nadhani *proposal* ambayo tumeileta tunaamini kwamba bado ni vyema ikabaki hivi hivi kwa sababu hata ukitizma tafsiri ya kiengereza inapelekea ni ile *mental disturbance* ambayo inatakikana na tisiangalie tu kwamba ulemavu wa akili ambao tunautizama ni ule wa moja kwa moja uko *directly* au *indirectly* na mto unaweza kuwa wa kudumu au ni wa *temporary.* Kwa hiyo, tutakapokwenda kujifunga namna hiyo tunaweza tukaondoa nadharia nzima ile ambayo tunaitaka tuikamate Mhe. Spika. *(Makofi)*

Lakini pia alizungumzia kifungu cha 15 cha mabadiliko haya kwamba kukwepa kodi kukoje isiwe moja kwa moja labda tuweke mipaka kuona kwamba ina *amount* maalum, ambayo pia ilizunngumziwa na Mhe. Saada Mkuya Salum.

Nadhani Mhe. Spika, tukijielekeza katika Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi wa Zanzibar ya mwaka 2012 kifungu cha 14(1) kinasema: Mtu yoyote ambaye kwa kitendo au kuacha kutenda anakusudia kukwepa kulipa kodi au anasaidia kukwepa kulipa kodi kwa njia yoyote katika njia zifuatazo:

(a) Kufanya hesabu za udanganyifu
(b) Kudanganya kwa kutoa nyaraka sahihi zinazohusiana na kodi."

Kwa hiyo, hicho kifungu ambacho kimewekwa hapa kina-*parameter* zake ambapo sheria mama inayohusiana na nadharia nzima ya kuzuia rushwa imeeleza. Kwa hivyo, ili huyu mtu ambaye anatajwa hapa hana dhamana anahitajika aingie katika mabano ya ile sheria ambayo nimeitaja ambayo ni Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ya mwaka 2012 kifungu cha 44.

Lakini pia matumizi mabaya ya *money* Mhe. Spika, nayo pia sheria ya *ZAECA* kifungu cha 43 imetaja. Kwa hiyo, ili huyu mtu asiwe na dhamana kwanza ku-*establish* kosa ambalo limetajwa na sheria mama hii ya *ZAECA* imetaja hili kosa kifungu cha 43. Kwa hivyo, ili awe ni mtu ambae hapewi dhamana kwa mujibu wa mapendekezo ambayo tumeyatoa lazima *qualify* yale maelezo Mhe. Spika, ambayo yameelezwa katika kifungu cha 43 cha sheria ya *ZAECA*.

Vile vile, alizungumza mabadiliko katika kifungu cha 151 kianze na maneno hayo nadhani wakati mwengine Mhe. Spika, ni ule namna ambavyo tunaandika sheria na nadhani kwa kile kifungu cha 151(2) tusianze pale ambapo tumeanza nadhani si sawa tungependekeza kibaki kama kilivyo. Lakini pia ameenda 151(3) kwamba neno hakitokuwa kikubwa iondoke.

Nadhani kinachotakiwa hapa kwa ile ya kiengereza imetumia neno *excessive* tunachotaka maana yake mahakama itakuwa *very reasonable* kuona *nature* ya kosa ambalo limefanywa na kwa namna gani kwa kosa hilo ambalo limefanywa na lina dhamana kiwango cha hiyo ambayo inatolewa dhamana kiweze kutolewa. Kwa hiyo, ni vyema tukaiachia mahakama na vile vyombo kwa kupima kosa lililotendeka ambalo ni *bailable* na kuona namna gani ambavyo kinampa dhamana. Haiwezi kufikia kwamba dhamana hiyo ikatolewa chini ya pale ambapo inatakiwa, haidhuru Mhe. Spika, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma alinambia kwamba tunapofanya marekebisho ya kifungu tunakuwa *intotality*.

Lakini mimi Mhe. Spika, wazo langu na pendekezo la hoja yangu ilikuwa inajielekeza katika kifungu cha 151 cha makosa ya jinani. Lakini pia kufuta kile kifungu ambacho kinampa Mhe. Jaji Mkuu lakini pia kifungu cha 200 ambacho kipo katika issue za *interpretation*. Kwa hiyo, si dhani kwamba kwa sasa hivi hakitokuwa kikubwa kwamba itaweza kuleta tatizo ni *excessive* maana yake unapima kosa ambalo limefanyika na ile *amount* ya dhamana ambayo inaombwa iwe tuna-*equate* vizuri isionekane kwamba dhamana ni kubwa sana kulikoni kosa ambalo limetendeka.

Kifungu cha 151(4) kama ambavyo nimesema mwanzo Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum nae ametoa mapendekezo yake ambapo ameyaona mambo ni mengi na kama nilivyosema awali Mheshimiwa yako mengi lakini ili ukitaka ku-*balance* vizuri tuyaangalie ni makosa mangapi ya jinai na makosa mangapi yamewekwa hapa hayana dhamana. Kwa hakika bado ni machache na yamewekwa kwa minajili maalum kulingana na wakati ambao tunao.

Lakini pia mahitaji ya mali inahitaji maelezo kama nilivyosema Mhe. Spika, ni maelezo ya vifungu vya sheria vilivyomo ndani ya Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ya *ZAECA*. Kwa hiyo, haihitaji maelezo ya kina hayo yaekwe katika mwenendo wa jinai, lakini sheria mama inayohusiana na makosa hayo yote imeyaweka.

Pia 153 hakitokuwa kikubwa nimekitolea ufafanuzi na ile ya 44(5) anaweza wanahisi kwamba tutaipimaje. Nadhani lengo la kuleta mabadiliko haya ya sheria hii ya mahusiano ya sekta binafsi na sekta za umma ni kuhakikisha kwamba tunaamsha hisia, tunaamsha muamko wa sekta binafsi kuingia ku-*inject* katika uchumi wa Zanzibar. Tumeona sheria ambayo kabla ya marekebisho

haya tuliyoyawasilisha hapa inavikwazo vingi ambavyo inazuia hasa katika miradi ya *unsolicited* na *solicited*.

Kwa hiyo, marekebisho hayaa ambayo tunayaweka na kwa hakika vigezo ambavyo tumeviweka ni dhahiri kwamba tunaamini na hasa tukiamini kwamba viongozi ambao watakuwa wanaisimamia wataleta tija katika kuhakikisha kwamba muwekezaji yote ambaye ana mradi wake ameuasisi mwenyewe na kwa hakika amefuata mapendekezo ambayo wametajwa ndani ya sheria anapewa nafasi, ili kuhakikisha kwamba yanatendeka yale serikali ya awamu ya nane inategemea katika kuhakikisha kwamba inawaletea maendeleo wananchi wake.

Lakini pia Mhe. Saada Mkuya Salum alizungumzia kuhusiana na kifungu cha 44(c) kama kitawekwa kwenye kanuni au laa. Mimi ningeshauri kwamba kibaki kama kilivyo kwamba kanuni iweze ku-*determine* na tuna sababu kwa nini iwe hivi. Tutakapokuja tukai-*confine* katika sheria huku wakati mwengine tunaweza kuja kutaka kufanya mabadiliko ikawa tabu na hii sasa hivi inaenda na kubadilika hata iliyokuwepo mwanzo *negotiating team* si ya hivi sasa. Kwa hiyo, tutakapokwenda kuiweka kwenye sheria humu ni wazi kwamba itaenda isiyakisi yale mambo ambayo tunayoyataka na niwatoe tu wasi wasi Mhe. Spika, hii ni kamati ambayo Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Hussein Ali Mwinyi yeye mwenyewe sasa hivi imeshaundwa chini ya mwenyekiti wake wa Mhe. Mwanasheria Mkuu mimi mwenyewe na watu wapo. Kwa hiyo, na tuamini wale ambao watapewa dhamana hizi na ni dhahiri kwamba serikali haitumuangalia tu huyo waziri akafanya anavyotaka lakini wazi kwamba serikali kuu itakuwa ina m-*monitor* nini ambacho atakuwa anafanya.

Mhe. Spika, nadhani nimejaribu vya kutosha sana  kuyajibu. Lakini kipekee niseme tu kwamba tumeyapokea mapendekezo yote ambayo yametolewa na kamati na kwa hakika nipongeze sana Mwenyekiti na kamati yake wamaetupa mapendekezo ambayo mazuri na tumeyabeba kadri ambavyo na lengo ni kuhakikisha kwamba mswada huu unakwenda kuakisi yale ambayo tunataka na yale ambayo ya awamu ya nane inataka kuyafanya kwa manufaa mapana ya nchi yetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, naafiki.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa. Naomba sasa niwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*).

*(Hoja ilitolewa imaliliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Spika:** Naomba sasa nimwite tena Mhe. Mwanasheria Mkuu ili aje atoe taarifa hapo.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria, ili kuupitia mswada huu kifungu kwa kifungu natoa hoja Mhe. Spika.

**KAMATI YA KUTUNGA SHERIA**

**Mswada wa Sheria wa Kurekebisha Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora ndani yake**

**SEHEMU YA KWANZA**
**Masharti ya Awali**

Kifungu 1 Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake

Kifungu 2

**Mhe. Mwenyekiti:** Samahani Mhe. Mwanaasha Khamis Juma uwahi kidogo maana yake ukichelewa tukikipitisha.

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia katika kifungu hichi cha151(3) nimshukuru kwanza Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa majibu yake ...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa kifungu cha kwanza tupo. Tunaendelea Waheshimiwa.

Kifungu 2 Marekebisho ya sheria mbali mbali.

**SEHEMU YA PILI**
**Marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai**
**Nam. 7 ya Mwaka 2018**

Kifungu 3 Kusomwa

Kifungu 4 Marekebisho ya kifungu cha pili pamoja na marekebisho yake

Kifungu 5

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilimuomba Mwanasheria Mkuu atupe ufafanuzi *exception* au *remedy* ya wale ambao wananyima dhamana kwa yale makosa ambayo hayana dhamana kama yalivyoelezwa kwenye 151, pale ambapo watakuwa hawana hatia wamewekwa ndani kwa kukosa dhamana kwa sababu makosa walishitakiwa hayana dhamana, pale ambapo mahakama imekosa kuwatia hatiani. Vipi sasa serikali ita-*remedy* huo muda na maisha waliopoteza kukaa rumande ikiwa miaka mitano, sita wakati mahakama haijawatia hatiani.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Omar Seif Shaaban katika swali lake linalohusiana na *remedial measures* kwa wale ambao hawakupewa dhamana lakini kesi imeenda miaka mingi na tayari wameshapoteza vitu vingi.

Msingi wa majibu yangu utakuwa unajielekeza kwamba si nia kuhakikisha kwamba kesi inachukuwa muda mrefu na nadhani kwa ambacho tunakizungumza hapa na kwa ambako tunataka kwenda ni kuhakikisha kwamba kesi zinamalizika kwa wakati. Tunaweza kuwa tulifanya makosa huko ambako tumetoka lakini siku ambayo ya *law day* nikikumbuka Mhe. Jaji Mkuu alisema upangiwaji wa kesi kwa mahakimu na majaji ndio ambao itakuwa ni *motion* ambayo wanayokwenda nayo. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba ni matarajio yetu huko tunakokwenda hatutayaona hayo. Nakushukuru.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Mhe. Mwenyekiti, majibu ya Mwanasheria Mkuu sio *commitment* ya kisheria ni hoja hapa Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba anapopewa mtu kosa ambalo halina dhamana na tunafahamu *investigate mashinering* yetu ni dhaifu, kesi zinachukuwa muda mrefu kuchunguzwa *judgment* zinachukuwa muda mrefu kutolewa. Kwa hiyo *obviously* inakuwa wiki moja au wiki mbili na kuwa watu wanapoteza kazi kwa kupewa makosa yasiyokuwa na dhamana, kuna watu familia zinaparaganyika, kwa sababu tu wawekwa rumande kwa makosa yasiyokuwa na dhamana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu tunachotaka hapa aweke kwamba serikali iji-*comment* kwenye sheria kwamba pale ambapo mtu ambaye amewekwa ndani kwa kosa lisilokuwa na dhamana na amekaa muda mrefu au amekaa muda fulani basi mahakama isipomtia hatiani afidiwe huyu mtu ndio hoja.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, namfahamu sana Mhe. Omar Said Shaaban katika hoja yake hii, lakini vyema akatupa nafasi na akakubaliana na serikali ya awamu ya nane kwamba huko siko ambapo tunakotaka kwenda na pindipo ambapo tutakwenda kuliona kuwa ni tatizo kila kitu ni kufanya tafiti, tukiliona kwamba ni tatizo na kuna umuhimu wa ku-*cover* hizo haki za watu serikali haitoshindwa. Lakini kwa sasa ni vyema akatupa nafasi ili kuona kwa namna gani kuendeleza muendelezo wa kesi. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Mhe. Mwenyekiti, hichi kifungu sio kipya kifungu kipo kwa sasa hivi kimeshibishwa kwa kuongezewa makosa. Tunachosema ni *from my exprince* kwamba i-*text time* sasa hakuna sisi tunataka *remedial provision* iingizwe na hoja hapa ni kwamba kwa vyovyote vile...

**TAARIFA**

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, taarifa yangu najua Mjumbe anaezungumza hapa ni Mwanasheria aliebobea, lakini sheria tunzopitisha za Kiswahili na wanaosikiliza wananchi wetu waswahili basi ajikite zaidi katika kuelezea Kiswahili kuliko Kiingereza. Ahsante.

**Mhe: Mwenyekiti:** Mhe. Omar Said Shaaban endelea.

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, napokea. Mhe. Mwenyekiti, tunataka kifungu kinachotoa shufaa kwa wale waliotuhumiwa na sisi tunaopitisha hii sheria sasa, tuweke kifungu kinachohakikisha mtu ambaye amewekwa rumande kwa muda mrefu kwa makosa

ambayo hayana dhamana, basi pale ambapo Mahakama imekosa kumtia hatiani, na wakati wa kuchangia wachangiaji wameeleza kuna watu wanapewa makosa haya kwa kubambikiziwa na kuna sababu nyingi, tunayaona kwenye jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini sasa Mhe. Mwanasheria Mkuu asikubali kwamba tufanye hiyo *amendment* ya kuingiza hichokifungu kidogo, ili kuhakikishia kwamba kama mtu amepoteza basi kuwe na fidia, ili wanaowajibika kufanya uchunguzi na wanaowajibika kushtaki wawe makini kuhakikisha kwamba wakizembea basi huyo wanayemshtaki waliomfikisha Mahakamani atafidiwa na serikali na serikali itakuwa iko makini zaidi, ili kuhakikisha kwamba Mahakama nazo hazichukuwi muda mrefu katika kuwashtaki watu. Ahsante.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, nadhani sitatofautiana sana na maelezo yangu ya awali. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Omar Said Shaaban aiache serikali ianze, halafu tutakapoona kuna mahitaji hayo hatutosita kufanya hivyo. Ndio kwanza tunaanza kuna matatizo haya, ni vyema tukaya-*address* ipasavyo, tukayatatua ipasavyo. Mhe. Hamza Hassan Juma alimuelekezea Mhe. Omar Said Shaaban na mimi naona nisitie Kiingereza. Kwa hivyo, ni vyema kwamba akatupa muda katika hili. Shukrani.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe, tumeshamaliza mara tatu. Mimi ningeshauri tu Waheshimiwa, mkalichukua lile alilolizungumza Mhe. Omar Said Shaaban kwa sababu ni kweli na kwenye nchi za wenzetu wengine huko watu wanafidiwa katika masuala kama hayo. Mtu umemchukua umemuweka ndani, na makosa haya mtu kasingiziwa wakati mwengine wala hahusiki. Nafikiri serikali ilichukuwe hili mliangalie. *(Makofi)*

Kama serikali itakuwa inawafidia wale wanaohusika na uchunguzi wa hizi kesi watakuwa makini, kwa sababu haiwezekani wawe wanaitia serikali kwenye hasara. Kwa sababu wanaweza wakawa wanapanga watu tukamsingizie mtu ili baadae tukavune. Nafikiri ni jambo la muhimu sana serikali ilitizame.

Mhe. Mjumbe, linafanyiwa kazi hili na serikali. Kabla ya Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, nilimuona Mhe. Juma Makungu Juma.

**Mhe. Juma Makungu Juma:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza nianze kumpongeza Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa namna ambavyo katujibu, lakini inawezekana kalisahau swali moja ambalo niliuliza na ndio maana nimesimama kwa ajili hiyo ya kupata ufafanuzi ama jawabu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipengele hiki cha kifungu cha 151(1) yalitajwa makosa hapa ambayo hayana dhamana. Nikalisoma kosa moja la kuingilia kinyume cha maumbile na kunajisi mtoto wa kiume. Nikauliza kwamba ina maana tofauti ama moja. Nikaambiwa tofauti, lakini kwa nini mtoto wa kike hakutajwa.

Swali langu ni kwamba kosa la kumnajisi mtoto wa kike lina dhamana na kama halina dhamana linaangukia wapi kwenye makosa haya, naona wa kiume katajwa wazi wazi. Ahsante.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. Napenda kumjibu Mhe. Juma Makungu Juma. Nadhani kama ambavyo katika majumuisho yangu nilivyosema kwamba, makosa haya yametajwa, yamo kubaka, kuingilia kinyume cha maumbile na kunajisi mtoto wa kiume. Ina maana kuingilia kinyume na maumbile ina maana pana sana, kama ambavyo ilivyo, ina muingiza au inakwenda zaidi ya huyo mtoto wa kiume. Lakini je, itakapotokezea sasa mtoto wa kike, inayofuata pale pana neno kubakwa ambayo ipo, kwa hivyo nadhani nayo pia ingeweza ku-*capture* yale ambayo tunayataka.

**Mhe. Juma Makungu Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Mwanasheria Mkuu tena kwa namna ambavyo anatufafanulia, lakini tunataka uwazi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna sababu gani ya msingi ikiwa neno "kuingilia kinyume cha maumbile" linawahusisha wote mtoto wa kike na mtoto wa kiume. Kuna sababu gani ya mwanamme akawekwa hapa kunajisi mtoto wa kiume *as a specific* inaonekanwa ikashindikana kwa mtoto wa kike. Kwa hivyo, atakubaliana na mimi kwamba kama hii ya mwanzo ya kuingilia kinyume na maumbile inahusisha wote na huyu mtoto wa kiume tumtowe au tumuingize na mtoto wa kike.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, kwa tafsiri moja ambayo anaizungumza inaweza ikawa sahihi. Lakini kwa nadharia ya kutia msisitizo ndio ambayo tutai-*specify* hii baadae kunajisi mtoto wa kiume. Kwa hivyo, kule *scope* yake ni kubwa lakini huku pia tukasema kwamba yeye *specific* ndio ambaye aingie.

**Mhe. Juma Makungu Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba niseme *AG* ni mwalimu wangu kama ambavyo Mhe. Omar Said ni mwanafunzi wa *AG*. Sitaki kubishana naye, ila tusisubiri. Kwa sababu kama sasa hivi tumeingiza ya mtoto wa kiume kwa sababu ya matukio ambayo tunayasikiza kwenye mawio, sio vizuri tukasubiria mpaka na watoto wa kike tukaisikia kwenye mawio. Kama itakuwa kweli ina uhusiano huo kwamba haiingie kwenye kuingilia kinyume cha maumbile, basi tungemuweka kabisa na mtoto wa kike au tukaondosha *verge* hapa, kwa sababu hii inaweza ikaleta shida kwenye tafsiri ya sheria kwenye Mahakama. Nashukuru sana nadhani *AG* kasikia tuendelee.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mjumbe. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma.

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi. Wakati nikichangia kifungu namba 3 kuhusiana na kiwango cha dhamana kilichopangwa kwa kuzingatia mazingira ya kesi husika na hakitokuwa kikubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, sikupingana naye kwenye majibu yake, lakini nilitoa ushauri hakunijibu. Kwa sababu nimesema kwamba kifungu hiki kiweke jadweli ambalo litaainisha kiwango cha fedha kwa mujibu wa kesi husika. Nilikuwa na sababu kwamba kutokukiweka wazi kifungu hiki inawezekana kikatoa mwanya kwa upande wa polisi na halikadhalika Mahakama wakafanya vile wanavyotaka.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, kwanza kwa kukubaliana na mimi katika namna ambayo ya kukiweka, lakini nadharia ya

kuandaa jadweli, hiyo nadhani ni mamlaka ambayo itaamua. Kwa sababu kinasema kifungu, kiwango cha dhamana kitapangwa kwa kuzingatia mazingira ya kesi husika na hakitokuwa kikubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa wakati mwengine kila kesi ina *nature* yake, sio kwamba kila kesi hii ndio ambayo unaweza kusema kwamba ni kesi ile nyengine. Kwa hivyo, mazingira ya kesi ndio ambayo yatatofautisha na kuona namna gani dhamana ambavyo itakavyokuwa inaweka. Nadhani tu tungeweza kuamini bado hivi pasi na kuweka hiyo jadweli ambayo anaiomba.

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma:** Mhe. Mwenyekiti, *AG* anajua, mmoja katika watunga sheria ni Baraza la Wawakilishi na anajua kwamba *process* ndefu inaanza kutoka huko, lakini mwisho wa siku watungasheria ni sisi. Kwa hivyo, kile ambacho tunahisi kinafaa, na mimi nimesema hivi mbona kuna sheria nyengine zinaonekana wazi kama kiwango kiwango hiki kwa kesi hii kutakuwa na kiwango hiki.

Kwa hivyo, nimuombe tu Mhe. Mwanasheria kwamba hili ambalo nimelishauri aone kwa upana wake ili kuondosha ule mwanya, ambao nimesema hapo mwanzo kwamba Mahakama au polisi wanaweza chochote kikaingizwa ndani yake. Sasa inawezekana pia hapa likapita suala la rushwa. Pengine mtu anaweza kusema kwa kesi yako hii basi inawezekana iwe hivi. Kwa maana hiyo nilikuwa naomba ioneshe tu wazi kama itafaa nikiwa mmoja katika watunga sheria wa Baraza hili. Kama *AG* ataona inafaa basi akubaliane na mimi. Isije ikawa ilee, anatuletea tena hapa marekebisho ya kifungu cha 151 wakati tulikipigia kelele isiwepo dhamana.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, nadhani tulichukuwe halafu tukalifanyie kazi, ili tuone kwamba kwa mahitaji ya baadae yatakuwa yanahitajika.

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wajumbe wenzangu kumpongeza Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa ufafanuzi wa hoja ambazo tumeziwasilisha, amejitahidi kwa kiasi chake.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa wakati nilipochangia nilizungumzia katika kifungu cha 151, yule ambaye amemnajisi mtu mwenye ugonjwa wa akili. Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu iko pale pale. Kwanza Mhe. Mwanasheria amesema kwamba kuna ulemavu pengine wa muda mfupi. Mimi nitofautiane na yeye kwa sababu, Mhe. Mwenyekiti, hakuna ulemavu wa muda mfupi. Ukimuona mtu ana ulemavu wa muda mfupi ujuwe huyo ni mgonjwa anaendelea na matibabu, mwisho wa siku daktari atathibitisha kwamba mpaka hapa tulipofikia matibabu yake huyu hawezi tena kutibika, sasa pale anakwenda kwenye ulemavu. Kwa hivyo, anaposema kwamba watu wenye ulemavu wanaingizwa katika wagonjwa hili mimi sikubaliani nalo.

Mhe. Mwenyekiti, huko tunakotoka nyuma watu wenye ulemavu walikosa haki zao nyingi, kutokana na masuala yao kujumuishwa katika mambo mengine kama haya. Kwa hivyo, sioni kama kuna ubaya au Mhe. Mwanasheria Mkuu aniambie, kuna tatizo gani kuwaonesha hapa watu wenye ulemavu katika sheria hii, ili kuwasaidia kupata haki zao huko mbele, tutakapolifunga hili wanasheria ndio hawa.

Mhe. Mwenyekiti, tulitunga sheria kwa nguvu hapa, matokeo yake ikarudi huku. Ndio hii leo tunaifanyia marekebisho. Katika kifungu cha 151 hichi hichi ambacho ile sheria tuliyoipitisha ya mwaka 2018, ilieleza wazi wazi mwenye ulemavu wa akili. Sasa kuna sababu gani kutokurejesha hapa lile suala la wenye ulemavu wa akili ikasomeka wazi wazi na hii ikaonekana, kwa sababu hawa ndio ambao wanapa changamoto kubwa ya kubakwa. *(Makofi)*

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu kama hakuna kikwazo kuliingiza neno hapa la "ulemavu wa akili" basi suala la ulemavu lazima hapa lionekana, ili hawa watu mwisho wa siku wapate haki zao Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante. Mhe. Mwanasheria Mkuu nakumbuka katika mchango wake Mhe. Mwantatu Mbarak alisema kwamba ile ya Kiingereza iliyotafsiriwa iko sahihi au vipi. Lakini hii tafsiri yetu ya Kiswahili ndio imeliondosha hilo neno. Mhe. Mwanasheria Mkuu.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa niseme kwamba sikusema kwamba kuna ulemavu wa muda mfupi. Nilichosema ugonjwa wa akili upo ule wa kudumu ndio unaingia kwenye ulemavu na upo ule ambao tunaita *temporary* hilo ndio ambalo nimesema, haukuwa katika ulemavu wa muda mfupi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tulichosema hapa ni ugonjwa wa akili ambao tumeusema. Nadhani kinachotakikana tukienda kuweka katika nadharia nzima ulemavu wa akili, itakuwa tumekwenda ku-*cover* ule u-*permanent* tu basi, kwamba yule *severe* kafika moja kwa moja huyu maana yake. Lakini wapo ambao ni *temporary* na ambao wanapata vitendo hivi ndivyo ambavyo tunataka kuwa-*cover*. Kwa hivyo, ugonjwa wa akili ama ambao utakuwa maana yake wa *severe* ule wa kudumu ambao umepelekea ulemavu au hii hatua ya mwanzo ndio ambao wote tunataka tu-*cover* na kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, tunachokwenda kusimamia hapa ni kwamba huyu mtu anaweza hata akawa mtu mzima, lakini hajui nini ambacho anakifanya wakati anafanyiwa. Kwa hivyo, tutakapo thibitisha kwamba wakati kitendo hicho amefanyiwa kutokana na athari za kiakili katika mazingira yote mawili, basi ni wazi kwamba mtu huyo atakuwa amelifanya kosa hilo Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis:** Mhe. Mwenyekiti, sipingani naye Mhe. Mwanasheria Mkuu, lakini ninachomuumba sitaki hata kwenda kwenye kura. Ninachomuomba kwa maslahi ya watu wenye ulemavu kupata haki zao, tusiwaingize kwenye wagonjwa hawa sio wagonjwa. Itafika siku huko katika kesi kama imeelezwa ugonjwa akifika Mahakamani ataambiwa apeleke cheti, na mwenye ulemavu wa akili hatokuwa na cheti, atakayekuwa na cheti ni yule mgonjwa ambaye anakwenda hospitali anapatiwa matibabu anarudi, cheti chake kipo. Mwenye ulemavu wa akili huwezi kukuta cheti chake Mhe. Mwenyekiti. Kwa kumnusuru kupata haki zake kwa nini tusiingize hapa.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, hoja yake inaweza ikawa ina mantiki kubwa, lakini tutakapoanza kufungua hilo la kuingiza kila mwenye ugonjwa wa ulemavu ina maana vinaweza vikaingia vitu vingi. Kwa hapa kwanza ambacho tumetaka tuki-*capture* ni mtu mwenye ugonjwa wa akili, hizo *disorders* ni nyingi mno zilizopo. Kwa hivyo, tulichokuwa

tukiki-*capture* hapa ni ile nadharia kwamba wakati hilo tendo linafanyika huyo mtu hakuwa mwenye akili timamu, na ndio hiyo *concept* ambayo tulikuwa tunataka tuikamate Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis, umeridhika au. Taarifa samahani Mhe. Omar Said Shaaban.

**TAARIFA**

**Mhe. Omar Said Shaaban:** Mhe. Mwenyekiti, nafikiri *amendment* ya kwenye *criminal procedure* au sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai kwenye hiki kifungu cha 151, imeyachukua majina ya makosa kama yalivyo kwenye *Penal Act,* kwa maana sheria ya makosa ya adhabu. Kwa hivyo, itakuwa ni *wrong* kuifanyia *amendment* hicho kifungu, kwa sababu tukirekebisha maana yake kosa hilo litakuwa halipo kwenye *Penal Act*. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, aridhike kama kuna haja ya kulifanyia marekebisho kosa lenyewe tuliite jina jengine, basi amendment iende kwenye *Penal Act* na sio kwenye *criminal procedure.* Shukrani. *(Makofi)*

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, namshukutu sana Mhe. Omar Said Shaaban, na kwa sababu tunayoifanyia marekebisho ni sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai namba 7, sio ile *Penal Act* ambayo ipo. Tukihisi nadharia kosa hilo nalo liingie katika makosa, nalo tutapata muda ambao tutaliingiza, lakini kwa sasa hivi tunakwenda ku-*capture* yale ambayo tu, huu ni mwenendo tu inachukua makosa katika sekta mbali mbali ambazo imeelekezwa kisheria.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis, nadhani utakuwa umelielewa vizuri zaidi nafikiri wameliweka vizuri.

**Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis:** Mhe. Mwenyekiti, nimelielewa lakini hata hivyo sijaridhika twende tu.

Kifungu cha 5 Kufuta na kuandika upya kifungu cha 151 pamoja na marekebisho yake.

**SEHEMU YA TATU**

**Marekebisho ya Sheria ya Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Namba 8 ya Mwaka 2015**

Kifungu cha 6 Kusomwa.

Kifungu cha 7 Marekebisho ya kifungu cha 2.

Kifungu cha 8 Marekebisho ya vifungu vya 3(1), 13(b), 13(c), 13(d), 14(1)(b), 15(a), 19(7), 19(8), 25(1), 38(5), 38(6), 38(7), 38(8), 38(9), 46(1), 46(3)(b), 46(3)(b)(i), 59(1) na 67 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 9 Marekebisho ya kifungu cha 9 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 10 Marekebisho ya kifungu cha 14(1).

Kifungu cha 11 Marekebisho ya kifungu cha 15.

Kifungu cha 12 Marekebisho ya kifungu cha 20 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 13 Marekebisho ya kifungu cha 30 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 14 Marekebisho ya kifungu cha 38 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu cha 15

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, lakini nilipokuwa nikichangia katika kifungu cha 15 marekebisho ya kifungu cha 44(9), waziri anayehusika na mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi anaweza kutengeneza kanuni zinazoelezea taratibu za uwekaji na ulipaji wa dhamana iliyowekwa chini ya kifungu kidogo cha 7.

Mhe. Mwenyekiti, nilimuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu hapa neno hili "anaweza" liondoke na liwekwe neno "atengeneze kanuni" badala ya anaweza. Kwa hivyo, na hili Mhe. Mwanasheria Mkuu aje anipe ufafanuzi wake.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, nadhani pendekezo la Mhe. Mwanaasha Khamis Juma hapa hapa lipo. Katika sheria unaposema neno "anaweza" maana yake *may* inaweza kuwa *shall*. Kwa hivyo, nadhani katika utendaji bora wa sheria hii itakapoonekana kwamba pana mahitaji hayo basi ni wazi kwamba atafanya.

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani utakuwa una kumbukumbu vizuri katika eneo hili mara nyingi *AG* huwa wanatuambia hivyo, lakini katika utekelezaji wake unaonekana kwamba ni hafifu. Sasa nimuombe, tunajua kwamba tumekasimu madaraka Baraza la Wawakilishi kwenye kanuni kuwapa mawaziri watunge hizo kanuni.

Lakini katika hili na nilinukuu kifungu cha 44(c), ili kazi ziweze kufanyika vizuri badala ya "anaweza" iwekwe "atengeneze" yaani ioneshe moja kwa moja kwamba atengeneze sio "anaweza", kwa sababu kwa hoja yake hiyo aliyosema hapo hapo ndio anachukua kwamba waziri inawezekana akafanya au asifanye, vyote vinatokea na hizo kanuni zinakuwa zinachelewa Mhe. Mwenyekiti, na hata katika moja, kipindi kilichopita mimi nilikuwa ni Mjumbe kwenye Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo. Kwa hiyo, haya pia tuliyakuta kanuni zinatungwa sheria tayari inafanyakazi lakini kanuni zake zinakuwa bado matokezeo yake inakuwa inatoa shida katika utekelezaji wa sheria.

Kwa hiyo, nimuombe Mhe. *AG* sana kwa hili halina madhara aweke tutengeneze ioneshe wazi haina tatizo lolote *AG* tufanye hivyo iwe wazi basi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. *AG* naona Mhe. Mwanaasha Khamis Juma anabembeleza kidogo, haya Mhe. *AG*.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Mwanaasha Khamis Juma kwa namna ambavyo amekuwa akiibembeleza serikali ikubaliane na hiyo. Lakini hiyo hiyo ambayo yeye amekwenda kuinukuu ya *Interpretation of the Law and General Provision Act* ya namba 7 ya 1984 kifungu 4 ndilo hilo ambalo nimesema *may to be construed as premissive* kwa hiyo, nadhani wakati mwengine tunapotunga hizi sheria tuamini wale ambao tunawapa madaraka na kilingana na mahitaji watafanya yale ambayo yanahitajika nashukuru.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mwanaasha inaonekana ameridhika, yupo bado haya.

**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma:** Mhe. Mwenyekiti, hakubaliani na mimi lakini na mifano nimetoa nimo katika Sheria Ndogo Ndogo tunaona changamoto hizo Mawaziri wanakuwa hawako *committed* katika kutunga hizi kanuni lakini kama anahisi mara hii kwa awamu hii watakuwa na mwendo kasi basi tuendelee.

Kifungu 15 Marekebisho ya kifungu cha 44 pamoja na marekebisho yake.

Kifungu 16

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi wakati ninachangia nilichangia kuhusiana na Kifungu hiki cha 44(c) ambacho itakuwa kinaunda timu ya majadiliano ya serikali na imeelezea yatakuwa na muundo, majukumu na uwezo wa kama ambavyo itaelezwa katika kanuni.

Kwa kweli, nilimuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba *Government Negotiation Team* (*GNT)* tuiunde kupitia sheria hii na *my argument was very simple* ni kwamba sisi ndio ambao tunatunga sheria *basically* na tulikuwa tunataka tujue hao ambao wapo katika *GNT* hiyo ni kina nani ili tuwezewe kuwa-*scrutinized* zaidi na hoja yangu ni kwamba tunakwenda sasa katika utaratibu ambao utakuwa unaleta maendeleo na kwa sababu *funding* duniani kote zimekuwa *very limited* hii ni *approach* ambayo kwa Zanzibar itakuwa kama *well*, tunaweza tukasema mpya kidogo…

**Mhe. Mwenyekiti:** Mheshimiwa tujitahidi sana Kiswahili maana yake kuna Waheshimiwa wawili hapa hawapo *comfortable* sana. hawana raha Mnadhimu mmoja yuko mbele yako hapo *(makofi)*

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** sasa nilikuwa nataka, nikushukuru Mhe. Mwenyekiti tuna sheria zote mbili hapa, mara ngenyinge tkitaka kujenga hoja unajua unatafuta maneno mazuru zaidi samahani sana. Nilikuwa nimemuomba Mhe. Mwanasheria sasa hii *team* ambayo ni team ya majadiano ya serikali tuiunde kupitia sheria hii na hoja yangu ni kwamba tukiunda kupitia sheria hii tutaweza kuisimamia zaidi, kwa sababu sisi kama Baraza la Wawakilishi ndio tunaotunga sheria. Lakini sisi ndio wasimamizi vile vile wa utekelezaji wa sheria tuiunde kupita

humu, ili tuone sasa nani na nani wanaingia katika Timu ya Majadiliano ya Serikali ambayo pamoja na mambo mengine.

Kwa kweli, timu ya majadiliano ya serikali haiangalii miradi ya *PPP* tunazo timu za majadiliano ya serikali ambayo tutakuwa tunaangalia mikataba sasa hivi tutakwenda *Oil and Gas Economy* bado hii itakuwa inafanya kazi hizi sasa tutakuwa tutengeneze hiki kifungu ambacho kitaonesha *composition* ya hiyo *Government Negotiation Team*.

Mhe. Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mzuri sana hapo Mhe. Rais hajakosea, lakini sasa tunataka tupate *content* nzuri zaidi, ili sisi kama tunaotunga sheria tuwe tuna wajibu zaidi kwa hizi timu ambazo zinaundwa, nakushukuru.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum lakini nadhani maelezo yangu hayatofautiani na awali.

Kwanza, ni vyema tukazipeleka kwenye kanuni nimejaribu kutoa sababu pale tutapo zi-*confine* huo muundo kila kitu ndani ya sheria hii tutakapotaka kuja kubadilisha inaweza ikawa tabu na vikao vya Baraza vina mpangilio maalum. Kwa hivyo, ni vyema tukaanza na niliwambia mwanzo kwamba niwatoe hofi nadharia nzima ya muundo pamoja na uteuzi wa Wajumbe hili ni wazi kwamba hata hiyo iliyotungwa sasa hivi iko katika mikono salama kuhakikisha kwamba ambao wamo wanatekeleza yale ambayo. Kwa kulisema hili hii *Government Negotiations Team* kwa sasa Mwenyekiti ni Mwanasheria Mkuu Wajumbe ni Katibu Mkuu Uwekezaji, Katibu Mkuu Fedha, lakini pia *DG* au *MD* wa *ZIPA* ikiwemo na kumualika Katibu Mkuu mwenye Mradi ambaye anahusika. Kwa hiyo, hii imeunda na bila shaka inabadilika nilisema mwanzo *Government Negotiations Team* iliyokuwepo mwanzo sio ya sasa.

Sasa tutakapokuwa kwa mfano, tunakuja nayo hii tunataka marekebisho ile ya sheria ina maana ingeeleza kwanza kuja na mabadiliko haya ambayo yapo. Lakini kwa kanuni itakuwa rahisi zaidi Mhe. Mwenyekiti, kufanya mabadiliko hayo nakushukuru sana.

**Mhe. Dkt.Saada Mkuya Salum:** Mhe. Mwenyekiti, ni sawa sawa hicho ambacho Mhe. Mwanasheria Mkuu anakizungumza ni kwamba hiyo *Government Negotiations Team* yeye ndio anayeijua na hii mimi *proposal* yangu hata niliyoweka sio kwamba yeye ataondoka kuwa Mwenyekiti, na hatuna nia hiyo, hapana *actually component* ambayo mimi nime-*propose* na naomba tuikubali ni kwamba hata hiyo *component* ambayo imo na tutaiweka katika sheria atakuwa Katibu Mkuu Hazina, Katibu Mkuu anayehusika na masuala ya Uwekezaji, Mkurugenzi Mkuu wa *ZIPA*, Mthamini Mkuu wa Serikali, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, katika vifungu vingine inabidi lazima tujue ile thamani ya mradi ambao yule muwekezaji anataka kuweka. Kwa hivyo, vile vile tunataka kumuingiza Mthamini Mkuu wa Serikali na Mwanasheria Mkuu wa *weather* yeye atakuwa Mwenyekiti, au vipi.

Lakini, vile vile kiifungu kinachofuata kiongezwe kiseme kwamba hiyo kamati inaweza ikamualika afisa mwengine yoyote anayeonekana anafaa kwa mustakabali wa mradi mwenyewe. Ili hili litakuwa vizuri likikuwemo kwenye sheria, unajua Mwanasheria Mkuu bila shaka na ndio ilivyo sasa hivi *speed* ya serikali iko kubwa *concept* pamoja na *approach* imebadilika

utekelezaji. Lakini hatutungi sheria kwa sababu ya Serikali ya Awamu ya Nane, tunatunga sheria kwa miaka 1,000 au 2,000, itakayo kuja kwa manufaa na maslahi mazima ya Zanzibar na hili litaingi katika *record* kwa nini sasa tusitunge sheria, tuangalie *forward looking* twende mbele zaidi sio kwamba tukitaka kuja kumueka mwengine hapa Baraza la Wawakilishi kurekebisha hapana. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, tuweke kipengele ambacho huyo Mwenyekiti au kamati yenyewe inaweza ikamualika mtu mwengine yoyote atakaingia katika kamati yengine yoyote kwa hivyo, hii iwemo katika sheria, kwa sababu sisi tunataka usimamizi zaidi na tunakwenda sambamba yeye anatuaminisha hivyo, na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunataka twende hivyo. Hata sisi Baraza letu Mwenyekiti limebadilika tunataka uwazi kabisa na twende katika kasi kama inavyokwenda Serikali ya Awamu ya Nane.*( Makofi)*.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru tena lakini nadhani hiyo nadharia ya kumualika mtu yoyote ndio imo ndani ya muundo na majukumu na uwezo ni kitu muhimu sana. Mhe. Mwenyekiti, lakini tumesema haya yote yakaeleze ndani ya kanuni kwa hiyo, huko katika kutekeleza majukumu yake na itakapoona haja hiyo kwa hakika wazo lake tumelichukua na litaekwa katika uundwaji wa kanuni nakushukuru sana.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Mhe. Mwenyekiti, sina shida na wala sioni tabu, hicho kipengele ambacho kipo kwenye kanuni kiingie katika sheria, ili sote tuwe tunakwenda sawa sawa najua hakuta haribika kitu tunamuamini sana, tunaamini Kamati, lakini Baraza lako lina-*mandate* ya kutunga sheria tunaomba hicho kitu kiwepo hapa maana hakina dhara yoyote. Sasa sisi huko kwenye kanuni wao ndio wanajua na wao ndio wanaona tunaiamini sana serikali tunamuamini sana Mwanasheria Mkuu. Kwa hiyo, tunatunga sheria kwa miaka ya mbele zaidi si kwa sababu leo yupo yeye na mwengine yupo tunatunga sheria, ili hata hao wanaokuja waone kwamba hizi sheria zimekaa sawa sawa kwa ajili ya utekelezaji. Naomba Mwanasheria msikivu, ngoja na mimi nibembeleze kidogo kama alivyofanya Mhe. Mwanaasha.

Mwanasheria tunaomba iingize hii katika sheria, ili tufanye vizuri zaidi najua atalikubali hili tuende mbele zaidi nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na ubembelezaji wa Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum kama amekubali ile ya mwanzo kwamba muundo, majukumu na uwezo uingie kwenye kanuni maana yake sheria za uandishi zinataka hata hicho ambacho unachosema kumualika mtu ni wakati wa kutekeleza yale majukumu. Kwa hiyo, kama inaenda kuonekana kwenye kanuni pia na hiyo inahitaji ikaonekane kwenye kanuni. Sasa ikiwa muundo umeupeleka kwenye kanuni halafu hapo unasema hivyo, sio utungaji mzuri wa sheria wala kanuni Mheshimiwa. *( Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum siwezi kukupa tena mara ya tatu naomba tuendelee, lakini bado utakuwa na nafasi ya kukaa na Mwanasheria Mkuu ili kusisitiza huko kwenye kanuni sasa maana huko ndio kwenye mitego yote huko. Maana kanuni zenyewe hazipo wakati mwengine, yaani sheria ipo kanuni hazipo zinachelewa kutungwa hasa tunaendelea Waheshimiwa.

Kifungu 16 Kuongeza Kifungu kipya cha 44(a), 44(b), na 44(c) pamoja na Marekebisho yake

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Spika:** Tukae Waheshimiwa, Mheshimiwa mtoa hoja Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake. Sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:** Mhe. Spika , naafiki.

**Mhe. Spika:** Ahsante, Waheshimiwa naomba niwahoji wale wote wanaokubalina na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

*( Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbali Mbali 2021**

*(Kusomwa kwa mara ya tatu)*

**Mhe. Mwanasheria Mkuu**: Mhe, Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Kurekibisha Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti bora ndani yake usomwe kwa mara tatu. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Spika, naafiki

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa hoja imetolewa naomba niwahoji tena wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mheshimiwa wanyanyue mikono wanaokataa, waliokubali wameshinda .

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)*

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, hatua hiyo sasa ndio imekamilisha *process* yetu ya kisheria na hapa sasa kilichobaki ni saini ya Mhe. Rais ili sasa iwe sheria kamiliki hii, kwa hiyo tutakuwa tumemalizia hapa.

Kwanza naomba nichukue nafasi hii kuishukuru sana serikali kupitia Mwanasheria Mkuu kwa namna ambavyo alivyowasilisha na namna ambavyo Wajumbe walikuwa wanajaribu kurekebisha baadhi ya maeneo na namna ambavyo Mhe. Mwanasheria Mkuu alikuwa anajaribu kuhakikisha sheria iende kama walivyokuja nayo serikali. Tunawashurukuru sana Waheshimiwa Wajumbe changamoto na michango yao ni mizuri sana.

Waheshimiwa Wajumbe kabla ya hapo naomba nimwite katibu *order paper* najuaimemaliza.

**Mhe. Spika:** Ahsante Waheshimiwa kwa kuwa shughuli zimekamilika naomba nitoe matangazo kwanza kabla sijaakhirisha shughuli zetu za Baraza. Nina matangazo machache, Waheshimiwa kwanza kuna tangazo la Waheshimiwa Wawakilishi wanaotoka Mkoa wa Kusini Pemba tutakapotoka humu wao wanaobwa wabaki kuna jambo muhimu linataka kujadiliwa.

Baada ya hapo nina tangazo jengine ni Waheshimiwa Wajumbe napenda kuendelea kuwakumbusha kuhusu semina za mafunzo tulizozipanga katika mkutano huu wa Baraza. Semina zetu zitaanza mara baada ya kuahirishwa kikao chetu cha Baraza cha asubuhi hii, juzi tulianza na baadhi ya semina zetu muhimu zinazo lenga kutoa mafunzo muhimu kwetu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ili tujielimishe kuhusu jumuiya mbali mbali za Kibunge.

Waheshimiwa Wajumbe, leo tutakamilisha semina zetu kwa semina kuhusu masuala ya mapambano zidi ya UKUMWI kwa mnasaba wa jumuiya yetu ya Umoja wa Wawakilishi wa Kupambana na UKIMWI Zanzibar (UWAKUZA), ambayo itatolewa na Tume ya UKIMWI Zanzibar. Hata hivyo, mbali ya semina hiyo pia tutakuwa na semina ya Masuala ya Itifaki kutoka Idara ya Mambo ya Nje Zanzibar, semina hii nayo ni muhimu sana kwetu kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ili tuweze kutambua vizuri zaidi na itifaki gani muhimu za kuzingatiwa kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya matangazo hayo sasa naomba nitoe shukurani. Baada ya hapo sasa naomba kuakhirisha shughuli za Baraza mpaka kesho saa tatu barabara za asubuhi.

*(Saa 6:40 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka*
*tarehe 25/02/2021 saa 3:00 asubuhi)*